
# MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA NA ISIMUJAMII (SWALI LA TATU NA NNE KARATASI YA PILI) .

Kwa majibu wasiliana na Bi .Mariam -0746711892

Setbooks summarised notes,questions and vedios are available.Contact Mdm.Mariam-0746711892




For answer,prefer calling -0746711892(Mdm.Mariam)

# (MTIHANI 1-44)

## MTIHANI 1

a) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vielezi viwili vya silabi moja. (al. 2)

b i) Eleza maana ya sauti za likwidi. (al. 1) ii) Toa mifano ya sauti za likwidi. (al. 1) c) Ainisha mofimu: Lililoliwa (al. 3)

d) Eleza huku ukitoa mifano matumizi mawili ya kiambishi 'ji'. (al. 2)

e) Huku ukionyesha upatanisho wa kisarufi katika sentensi, weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka. (al. 2) i) Uwele

ii) Vita

f) Tumia 'O' rejeshi tamati kuunganisha sentensi zifuatazo. (al. 1)

Tawi limekauka

Tawi limeanguka

g) Tambua vivumishi na uonyeshe ni vya aina gani. (al. 3)

Wanafunzi wawa hawa waliochelewa watafanya kazi ya sulubu kama adhabu.

h) Kanusha: Msichana ambaye amefika ametuzwa. (al. 1)

i) Onyesha aina za virai katika sentensi hii: (al. 2)

Wale wazazi wetu watawasili kesho saa tatu.

j) Unda nomino kutokana na kitenzi 'Haribu' (al. 1)

k) Tambua aina za vitenzi katika sentensi. (al. 2)

Hawa sio wachezaji bali wamekuwa wakichezea timu hii.

l) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya viunganishi vya kulinganua. (al. 1)

m) Eleza matumizi mawili ya 'ka' . Toa mifano katika sentensi. (al. 2)

n) Andika visawe ya maneno yafuatayo (al. 2)

i) Daawa ii) Ainisha

o) Onyesha kwa kauli ulizopewa (al. 1)

i) Ja (tendewa)

p) Andika kinyume: Tajiri aliyesifiwa amelaaniwa. (al. 1)

q) Chananua sentensi hii kwa kutumia vishale. (al. 4)

Yule mgeni aliyefika jana ameondoka leo.



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

r) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (al. 2)

Oyula atapendwa na wengi ikiwa atashinda leo.

s) Eleza majukuma mawili ya chagizo huku ukitoa mifano. (al. 2)

t) Akifisha. (al. 3)

sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote kumbuka

u) Andika ukubwa wa sentensi katika wingi. Nyundo imo ndani ya kibweta. (al. 1)

ISIMUJAMII (ALAMA 10)

Eleza matatizo matano yanayowakabili wazungumzaji wa Kiswahili. (al. 10)

MTIHANI WA 2

a) Taja sauti moja ambayo ni kipasuo- kwaruzo hafifu cha kaakaa gumu (al.1
b) Tofautisha kati ya silabi wazi na funge, huku ukitoa mfano mmoja mmoja (al.2)
c) Eleza matumizi mawili ya kiambishi "li" (al.
d) Tunga sentensi mbili katika wingi ukitumia viunganishi vifuatavyo:(al.4)
   i. yamkini ii. labda
e) Huku ukitoa mifano mwafaka, onyesha maumbo matatu ya ngeli U-ZI. (al.3)
f) Onyesha vielezi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani. (al.2)
   i. Rajani alianguka mchangani pu!
   ii. Maria anapenda kurandaranda ovyo.
g) Hii sentensi ni aina gani? Thibitisha. (al.2)

Atakuwa akiimba na kurukaruka leo jioni,wageni waketipo mezani h) Ainisha mofimu katika neno hili .(al.4)

Aliyemchelewesha

i) Tunga sentensi mbili kwa kutumia aina mbili za virejeshi. (al.4
j) Iandike sentensi hii upya kwa kuanza na:kando ya barabara …

Mti mrefu umeanguka kando ya barabara . (al.2

k) Changanua sentensi hii ukitumia jedwali Ijapokuwa yeye ni mweusi tititi, ni mrembo mno.
l) Tunga sentensi katika umoja ukitumia kuhusishi cha hali. (al.2)
m) Andika sentensi hii kwa msemo wa taarifa:

"Enyi wanafunzi watundu, rudini nyumbani mwenu, mje kesho asubuhi na wazazi wenu," Mwalimu mkuu alisema kwa sauti ya juu. (al.3)

n) Nyambua vitenzi vifuatavyo kulingana maagizo katika mabano na kisha utungie sentensi katika hali uliyonyambua.(al.4) a) (kutendeka)
   b) (kutendana)

o) Onyesha aina za shamirisho katika sentensi hii.(al.3) Maria amelimiwa shamba lote na trekta

For answer,prefer calling -0746711892(Mdm.Mariam)

ya oira.

p) Andika nomino moja kutokana na kitenzi hiki (al.1)

Tatua

<u>ISIMU JAMII</u>

Aziz: Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways beba! 46 Adams mbao Kenyatta, railways!

Shiko : Namba nane ngapi?

Aziz: Mbao ingia,blue.

Shiko:Nina hashuu.

Aziz: Blue auntie.

Shiko :sina.

Aziz: Ngia 46! Adams mbao Kenyatta railways gari bebabeba!

Ahendera :Mimi sinako ishirini.chukuako tu kumi.

Aziz: Dinga inakunywaga petrol mzee.

Ahendera: kumi mingi.

Aziz: Haya ingia twende. Driver imeshona twende.

<u>Maswali</u>

a. Eleza muktadha wa mazungumzo haya (al.4)

b). Taja sifa sita za lugha iliyotumika katika mazungumzo haya .(al.6)

## MTIHANI WA 3

a) (i) Eleza jinsi kitamkwa /u/ kinavyozuiliwa (alama 2)

(ii) Andika tofauti moja kati ya sauti hizi. (alama 1)

/t/ na /d/

b) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mwanajamii yule alijibu maswali yote kwa makini.

c) (i) Eleza maana ya vitenzi vishirikishi. (alama 1)

(ii) Tunga sentensi moja moja kuonyesha aina mbili za vitenzi vishirikishi. (alama 2)

d) Yakinisha sentensi ifuatayo. (alama 1)

Mtoto hakufundishwa wala kupewa vitabu.



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

e) (i) Eleza maana ya silabi. (alama 1) (ii)

Huku ukitoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili. (alama 2)

f) Ainisha viambishi katika sentensi hii kimuundo na kidhamira. (alama 3)
Wataonana

(i) Kimuundo:

(ii) Kidhamira

g) Tumia nomino yoyote katika ngeli ya KU-KU pamoja na kiashiria kisisitizi cha karibu kutunga sentensi.

(alama 1)

h) Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali isiyodhihirika (alama 1)

i) Tunga sentensi mbili ili kubainisha maana za neno: Jinsi (alama 2)

j) Huku ukitoa mifano, eleza matumizi mawili ya alama ya kinyota katika uakifishaji. (alama 2)

k) Eleza miundo mitatu ya vishazi tegemezi na kuitolea mifano mwafaka katika sentensi. (alama 3)

(l) (i) Eleza maana ya shamirisho kipozi. (alama1)

(ii) Benta alimlimia mamake shamba kwa trekta. Anza kwa yambiwa (alama1)

(m) (i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao.

S – KN (N/Wθ) + KT (Ts+T+RH+E) (alama 2)

(ii) Changanua kwa matawi sentensi ifuatayo: (alama 2)

Kile chake kipya kinanipendeza mno.

(n) Eleza matumizi yoyote mawili ya kiambishi KU na kuyatolea mfano mmoja mmoja wa sentensi.

(alama 2)

(o)Tunga sentensi sahihi ukitumia kivumishi cha ki ya mfanano na kielezi cha namna kitumizi.

(alama 2)

(p)Tunga sentensi ukitumia kitenzi cha silabi moja kinachomaanisha kuogopa katika kauli ya kutendeka. (alama 2)

(q) Eleza maana ya:

For answer,prefer calling -0746711892(Mdm.Mariam)

(i) Papo kwa papo kamba hukata jiwe. (alama 1)

(ii) Ua langu la waridi limechanuka. (alama 1)

(r) (i) Tunasema baraza la wazee …………………cha kuni na ………………..…… ya nguo (alama 1)

(ii) Ajuza ni kwa mwanamke mzee na …………………ni kwa msichana mchanga ilhali shaibu ni kwa mwanamume mzee na ………………………ni kwa mvulana aliyebaleghe.

(alama 1)

ISIMUJAMII

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

Niaje wasee! Midterm ilibamba lakini ilkua fupi sana, tumerudi books, huu ni mwaka wa mwisho tujikaze jo. Msifikirie hizo hepi zetu ni reality, kuchill ni jambo la maana jo! ama niaje bro…hustle ni real, bidii ndio itatuokoa

(a) Tambua sajili inayohusishwa na kifungu hiki (alama2)

(b) Eleza sifa zozote **nne** za kimtindo zinazojitokeza katika kifungu hiki. (alama 4)

(c) Eleza sababu **nne** zinazosababisha matumizi ya lugha ya aina hii. (alama 4)

MTIHANI WA 4

(a) Taja vipasuo sighuna (alama 2)

(b) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: kirai nomino, kirai tenzi, kirai husishi (alama 2)

(c ) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi (alama 2)

Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo . (d) Sahihisha

Mwalimu mwenye alikuja jusi anafudisha Kiswahili vizuli. (alama 2 ) (e) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2

Hakuwapiga wala kuwalaghai.

(f) Eleza viambishi katika neno lifuatalo (alama 3)

Walichokilalia

(g) Bainisha vivumishi vilivyo katika sentensi ifuatayo: (alama 2)



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

Wanafunza wote wenye nidhamu watapewa tuzo kubwa na mwalimu wao. (h) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale (alama 4)

Yohana na Otieno hucheza kandanda.

(i)Andika sifa tatu zinazobainisha sentensi changamano. (alama 3)
(j)Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi. (alama 2)

Askari jela alimwuliza Kendi kama alidhani hapo ni kwao. Alimwamuru aende kwake mara moja.

(k) Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama 1)

IK+KI+KI+KI
(l) Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo. (alama 2)

(i) kibainishi

(ii)parandesi

(m) Tumia neno –baya kama: (alama 2)

(i) kiwakilishi (ii)kielezi
(n) Tunga sentensi sahili ukitumia kitenzi 'la' katika kauli ya tendewa. (alama 2)

(o)Badlisha maneno yaliyopigiwa mstari yawe vitenzi. (alama 2)

Yunis amepata <u>faida</u> kutokana na <u>ukulima</u>.

(p)Kwa kuzingatia maagizo andika upya sentensi ifuatayo: (alama2)

Tinga amewafanya ng'ombe wake wanywe maji.

(Anza kwa : Mifugo wangu …………..usitumie 'amewafanya')

(q)Onyesha miundo miwili ya nomino za ngeli ya U-U. (alama 2 )

(r) Bainisha maana mbili zinazojitokeza kutokana na sentensi hii. (alama 2) Umu

alimwandikisha mkewe.

(s)Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyodhihirika. (alama 1)

ISIMUJAMII

(a) Lahaja huainishwa katika makundi mawili. Yataje (alama 2)

(b) Eleza sifa zozote nne za lugha ya taifa. (alama 4)

For answer,prefer calling -0746711892(Mdm.Mariam)

(c) Tolea ushahidi namna nne kwamba Kiswahili ni lugha ya kimataifa. (alama 4)

## MTIHANI WA 5

a) Eleza sifa mbili bainifu za sauti /a/ (alama 2)

b) i) Mofimu ni nini? (alama 2)

ii) Ainisha mofimu katika kitenzi; (alama 2)
Alimwona

c) Andika kitenzi chenye muundo ufuatao; (alama 2)
Kiambishi ngeli, wakati uliopita, mzizi, kauli tendwa na kiishio.

d) Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha matumizi ya kiimbo. (alama 2)

e) Ziandike upya sentensi kulingana na maagizo yaliyo banwa. (alama 4)
i) Kijitabu kile kulirushwana kiranja. (Tumia kivumishi kisisitizi cha karibu) ii) Barabara nyingi zimesakafiwa. (Tumia wakati ujao hali ya mazoea)

f) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi (alama 4)
Cherotich aliwahakikishia wazazi wake kwamba angetia bidii katika masomo yake iliapite mtihani wake

g) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia rejeshi-amba (alama 2)
i) Mshukiwa alipelekwa mahakamani ii) Mshukiwa alichukuliwa hatua

h) Changanua sentensi ifuatayo kwa mtindo wa jedwali (alama 4)
Mto uliofurika mwaka jana uliwaua mamba wengi

i) Tambua shamirisho, chagizo nakihusishi katika sentensi (alama 3) Mgonjwa alitibiwa na daktari jana jioni.

j) Taja ngeli za nomino zifuatazo (alama 2)
i) Sandarusi ………………………………………… ii) Saa………………………………………………………

k) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)
Mamlaka makubwa ya Rais haya kwa zijuhudiza upinzani

l) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi kifuatacho (alama 2)
La

m) Tunga sentensi kudhihirisha maana za vitate vifuatavyo (alama2) i) Bure ii) Pure

n) Andika katika hali ya ukubwa wingi (alama 2)
Msichana mrembo ameolewa na mwanamume hodari.

o) Kamilisha tanakali za sauti zifuatazo (alama 2) i) Maji yalijaa………………………………………………………………………………………………
………….
ii) Barabara imenyooka
…………………………………………………………………………………………..

p) Eleza maana ya mzizi wa kitenzi (alama 1)


Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

ISUMUJAMII

a) Lugha rasmi ni nini? (alama 2)

b) Eleza sababu zozote tatu ambazo huenda zikamfanya mzungumzaji afanye makosa ya kisarufi na kimatamshi (alama 3)

c) Huku ukitoa mifano mwafaka fafanua sifa tano za sajili ya bungeni. (alama 5)

## MTIHANI WA 6

a) Taja mifano miwili miwili ya konsonanti ambazo:

i. Hutamkwa kama irabu (alama1) ii. Zinapotamkwa husababisha mrindimo wa nyuzi za sauti (alama 1)

b) Tambua viambishi ngeli vya nomino zifuatazo (alama 1) i. Kikaragosi

ii. Nyuzi

c) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi

Bwana Kizito ameenda Kisiwani kununua riwaya iitwayo Msimu wa Vipepeo. (alama 2)

d) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi mwafaka

Utakula limau? Utakula tikitimaji? (alama 2)

e) Badilisha vivumishi katika sentensi zifuatazo kuwa viwakilishi vilivyoonyeshwa mabanoni.

i. Mtoto mzuri ameniazima kalamu yake. (viradidi vya mbali kidogo) (alama 1)

ii. Mti mrefu utaliangukia jumba kubwa. (vya pekee vinavyoleta dhana ya ziada) (alama 1)

f) Kanusha sentensi ifuatayo

Mtoto alipomwona mama alifurahi na kumkumbatia. (alama 2)

g) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (alama 2)

Shamirisho kitondo, kitenzi, shamirisho kipozi, kivumishi cha umilikaji, kihusishi, kiima

h) Tunga sentensi ili kudhihirisha matumizi yafuatayo ya neno "li" (alama 3) i. Njeo

ii. Kitenzi iii. Ngeli

i) Andika neno lenye muundo ufuatao (alama 3) Kiambishi kikanushi cha nafsi ya tatu umoja, kiambishi kikanushi cha hali timilifu, kiambishi kiwakilishi cha yambwa, mzizi wa sauti moja, kiambishi cha hali ya kutendesha na kiambishi cha hali ya kutenda.

j) Tunga sentensi yenye kirai kielezi cha mamna kikariri na kielezi cha namna halisi. (alama 1)

k) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia vinyume vya vitenzi vilivyopigiwa mstari. (alama 2) Watu <u>walimdharau</u> kiongozi wao hadi akaanza <u>kubabaika</u>.

l) Tunga sentensi ifuatayo upya kwa kutumia nomino ya jamii badala ya maneno

For answer,prefer calling -0746711892(Mdm.Mariam)

yaliyopigiwa mstari.

Mchezaji alivishwa <u>mtungo mrefu wa maua</u> shingoni baada ya ushindi wake. (alama 1)

m) Tunga sentensi ukitumia kisawe cha neno “ kiroho”

n) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali ya kuendelea

Abdan anasafisha nguo zake vizuri sana. (alama 2)

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale

Watu wote walioalikwa mkutanoni wanajiandaa kusafiri.

p) Andika kwa msemo wa taarifa

Tetei! Njoo hapa nikutume sokoni,” baba alisema. (alama 2)

q) Tenganisha silabi katika neno lifuatalo kisha uonyeshe miundo ya silabi hizo. (alama 2)

Mbuni

r) Andika neno moja lenye sauti mwambatano za:

(alama 2) i. ufizi ii. midomo

s) Tunga sentensi mbili tofauti ukitumia kiambishi –ku- kuonyesha:

(alama 2) i. Wakati ii. Nafsi

ISIMUJAMII-ALAMA 10

a) Eleza maana ya lugha ya taifa (alama 2)

b) Fafanua sababu nne zilizosababisha Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha ya taifa nchini Kenya.

. (alama 4)

c) Eleza majukumu manne ya Kiswahili nchini Kenya. (alama 4)

## MTIHANI WA 7

a) Taja sifa mbili bainifu za irabu /u/ (alama 2)

b) Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru cha nafsi ya tatu umoja. (alama 2)

c) Andika umoja wa sentensi zifuatazo. (alama 2)

i) Wakitaka tuwasamehe waje watuombe radhi kwa waliyotufanyia.

ii) Yaliyosemekana kuwa ni yao yameharibiwa na binamuo

d) Yakinisha (alama 2)

Hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini.

e) Bainisha shamirisho **kipozi** na **kitondo** katika sentensi ifautayo. (alama 2)

Mama alimpikia mwanawe chakula alichokitamani sana.

f) Tunga sentnesi moja yenye chagizo ya mahali na ya wakati. (alama 2)

g) Onyesha mfumo wa sauti katika tungo: Mtumbwini. (alama 2)

h) Tambulisha vipashio vitatu vya sarufi ya Kiswahili. (alama 3)

i) Huku ukitoa mfano, eleza mantiki inayopatikana katika kauli ya kutendua. (alama 2)

j) Taja matumizi manne ya kiambishi "ki". (alama 2)



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

k) Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo. (alama 2)
Jambazi lilimwibia Okoth gari jipya.

l) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Nitaenda maktabani ingawa ninaumwa na kichwa.

m) Andika katika kauli ya kutendesha (alama 1)
Ile pombe aliyokunywa Chacha ilimfanya alewe.

n) Changanua kwa kutumia mtindo wa kielelezo matawi. (alama 4)
Mtoto ambaye amefika ni ndugu yangu.

o) Andika kinyume cha sentensi ifautayo. (alama 2)
Huzuni alisifu nduguye aliyekusanya takataka
zote. p) Tumia neno 'vibaya' kama:

i) kivumishi ii) Kielezi

For answer,prefer calling -0746711892(Mdm.Mariam)

q) Tunga sentensi yenye kihuhishi cha 'A' - unganifu katika ngeli ya U - ZI. (alama 2)
(alama 1)
r) Mbwa wetu amekatwa mkia. Geuza katika hali ya ukubwa.
(alama 2)
s) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya maneno haya.
(alama 1)
Mkembe, mkebe
t) Tumia ngali kutunga sentensi ili kuleta maana ya:
(alama 2) i) Tendo katika hali ya kuendelea ii) Tendo kutoweza kufanyika kwa sababu ya wakati kupita

ISIMUJAMII (ALAMA 10)

a) Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Toa sababu tano. (alama 5)
b) "….sote tunajua kwamba ni kudura. Makiwa!"
i. Tambua sajili iliyotumika katika dondoo hili.
(alama 1) ii. Eleza sifa nne za sajili hiyo.
(alama 4)

MTIHANI WA 8

MATUMIZI YA LUGHA : (ALAMA 40)

a) Tofautisha sauti zifuatazo ukizingatia uzuiliaji wa hewa. (alama 2)
i) ny
ii) y
b) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kubadili maneno yaliyopigiwa mstari kwa nomino.
Mwanafunzi mwerevu alitafakari
c) Tunga sentensi ukitumia '-ja' katika kutendewa. (alama 2)
d) Yakinisha sentensi ifuatayo katika ukubwa wingi.
Mtoto wa mjini hakunywa maziwa aliyopewa na msichana.
(alama 3) e) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo :
(alama 2) furahiwa
f) Andika sentensi ifuatayo katika msemo wa taarifa : (alama 2)
"Ninajitolea kwangu kuwapokea wageni hawa leo." Mwenye nyumba alisema.
g) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao : (alama 3)

i) nafsi
ii) yambwa
iii) mzizi iv)
kutendea v)
kutenda vi)
kirejeshi

h) Eleza uamilifu wa maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo.
(alama 2) i) Kazi <u>yoyote</u> itafanywa na mafundi hawa. ii) Kazi <u>yote</u> itafanywa na mafundi hawa.

i) Toa mfano wa sauti mwambatano ya kaakaa gumu. (alama 1)

j) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao : (alama 3)

N + V + V + E + t + N

k) Nomino zifuatazo ni za ngeli gani ? (alama 2)

i) kiu .......................................................................................................................................
..

ii) bidhaa ...................................................................................................................................

l) Eleza majukumu mawili ya sentensi ifuatayo :

Ondoka hapa na nikikupata tena nitakushtaki! (alama 2)

m) Tunga sentensi ukitumia kihusishi cha wingi wa ngeli ya I-ZI. (alama 2)

Mjomba alijengewa nyumba kubwa kwa mawe msimu uliopita

o) Tumia jedwali kuchanganua sentensi ifuatayo: (alama 4)

Dereva aliendesha gari ila utingo hakuwa analipwa nauli.

p) Tunga sentensi ukitumia wakati ujao hali endelevu. (alama 1)

q) Eleza matumizi ya ‘kwa’ katika sentensi ifuatayo: (alama 1) Mfungwa aliachiliwa kwa kubadili tabia zake.

r) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo:

Nyinyi mtapadiwa mbegu kwa jembe la mtwana huyu. (alama 3)

s) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya kinyota. (alama 1)

4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)

“Haya basi. Beba mmoja! Beba mmoja! Dada njoo. Nafasi ni ya mmoja. Ni mbao tu. Bei ya chini kuliko keki. Usiachwe, bei ni poa.”

a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya. (alama 2)

b) Fafanua sifa nane za sajili hiyo. (alama 8)

## MTIHANI WA 9

a. Taja na utofautishe sauti sighuna za ufizi (alama 2)

b. Taja ala za kutamkia zinazotumiwa kuelezea sifa za irabu yoyote ile. (alama 2)

c. Andika neno lenye muundo ufuatao wa vitamkwa. (alama 2

Kipasuo si ghuna cha mdomo + irabu ya mbele tandazwa + nazali ya mdomo + irabu ya kati tandazwa.

d. Fafanua tofauti iliyopo kati ya kiambishi na mofimu. (alama 2)

e. Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya vitenzi vya silabi moja katika jinsi ya kutendesha.

i. La ii. Nywa iii. Fa

f. Onyesha matumizi ya kiambishi ‘ki’ katika sentensi ifuatayo. (alama 2) Salim atakupikia chakula kitamu kisha upeleke kule chumbani.

g. Onyesha sauti mwambatano kwenye maneno yafuatayo. (½ x 4 = 2) i. Mandhari

ii. Kunywa iii. Vushwa

iv. Changamka

h. Huku ukitoa mifano miwili, fafanua miundo ya majina katika ngeli ya LI-YA. (alama 3)

i. Kanusha katika wingi. (alama 1)

Uliko ndiko kuliko navyo.

j. Tumia kihusishi 'katika' kwenye sentensi kuonyesha : (alama 2) i) Mahali ii) Hali

k. Bainisha vitate katika sentensi ifuatayo na ueleze maana yazo. (alama 2) Nyumba hio itahamwa na mbwa aliye na watoto wanaoamwa.

l. Akifisha sentensi ifuatayo kuonyesha usemi halisi. (alama 2) hewala amefaulu katika mtihani wake

m. Changanua vipashio vya kisarufi katika kiarifa cha sentensi ifuatayo : (alama 2)

Wanasagamoyo hawakupendana

n. Tunga sentensi na ubainishe namna mbili za uamilifu wa kundi nomino. (alama 2)

o. Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu. (alama 2)

Mama huwafulia watu nguo zao

p. Fafanua maana ya kirai, kisha utunge sentensi sahihi ambayo haina nomino kuonyesha kirai nomino.

q. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (alama 4)

Yule abiria aliyejeruhiwa vibaya alipelekwa hospitali kisha jamaa zake wakaarifiwa

r. Andika kinyume. (alama 1)

s. Sahihisha kwa kutumia kirejeshi cha mazoea. (alama 1)

Kambarau ambao iliyoundwa vyema haitatizi.

4. <u>ISIMU JAMII (ALAMA 10)</u>

a. Ukiwa mkaguzi mwalikwa katika mashindano ya Kiswahili, fafanua na kueleza mambo yanayochangia wanafunzi kufanya makosa ya kisarufi na ya kimatamshi katika lugha ya Kiswahili.

b. Eleza umuhimu wa Isimu Jamii. (alama 5)

## <u>MTIHANI WA 10</u>

a) Andika neno lenye :

i. Kikwamizo cha kaakaa gumu :……………………………………………. (alama 2)

ii. Kimadende:…………………………………………………………….



@. BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

b) Eleza maana ya kiimbo (alama 2)

c) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo : (alama2)

Waliwao.

d) Tunga sentensi kubainisha aina zifuatazo za maneno (alama 2

i. Nomino ya pekee ambayo ni kielezi cha wakati

ii. Kiwakilishi kimikilishi, nafsi ya pili wingi

e) Unda kitenzi kutokana na neno “ mcheshi” (alama 1)

f) Tunga sentensi katika wakati ujao hali ya kuendelea. (alama 2)

g) Kanusha

Mtegemea cha nduguye hufa maskini (alama 1)

h) Weka maneno yafuatayo katika ngeli mwafaka (alama1)

i. Uchina:…………………………… ii. Kiwavi:……………………………

i) Bainisha matumizi ya parandesi katika sentensi . (alama 2)

j) Andika kwa kinyume (alama 1)

Mtii sheria ni anayeishi ndani ya taifa husika

k) Andika sentensi katika hali ya udogo, wingi (alama 2)

Alishikwa na jipu ambalo lilivimbisha mguu mithili ya pera.

l) (i) Eleza maana ya sentensi changamano (alama 2)

(ii) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya vishale (alama 4)

Ingawa ametufunza mara nyingi, hatujaelewa somo hili

m) Ainisha shamirisho katika sentensi: (alama )

Baba yake alijengewa nyumba na mwashi stadi kwa matofali

n) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo : (alama 2)

Kalamu iliyonunuliwa jana jioni na mwalimu imepotea leo

o) Ainisha miundo miwili ya kirai kivumishi katika sentensi moja. (alama 2)

p) Bainisha matumizi ya –**po**- katika sentensi ifuatayo : (alama 2)

i. Sijui alipohamia lakini ajapo mwulize.

ii. Eleza matumizi mawili ya kiambishi –**u**- na uyadhihirishe katika sentensi. (alama 2)

q) Andika kwa usemi halisi (alama 4)

Kaka alisema angekuwa akienda shuleni kila mara kuwaona walimu wangu.

r) Andika kisawe cha neno **kisogo** . (alama 1)

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

1.Eleza matatizo **matano** yaliyokumba maenezi ya Kiswahili kabla ya uhuru nchini Kenya (alama. 5)

2.Fafanua sifa **tano** za lugha inayotumiwa darasani (alama 5)

## MTIHANI WA 11

(a) Toa mfano mmoja wa: (alama 2)

(i) Kipasuo

(ii) Kitambaza

(b) (i) Kiimbo ni nini?
(alama 1)

(c) Andika maneno yenye miundo ifuatayo ya sauti.
(alama 2)

(i) KIKKKI

(ii) IIIKI

(d) Kanusha sentensi ifuatayo:
(alama 2)

Amekuja kukuona na ataondoka kesho

(e) Andika katika usemi wa taarifa.
(alama 2)

“Hicho kijicho cha paka cheupe leo marufuku kwangu”. alisema mzee kambumbu

(f) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo (alama 2)
(i) Chuma
(ii) Zawadi
(g) Eleza matumizi mawili ya nukta pacha. (alama 2)
(h) Andika sentensi ifuatayo katika udogo wingi (alama 2
Uso wake umefura kabisa baada ya kuumwa na mbwa.
(i)Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi. (alama 4)
Mchezaji atakayeshinda atatuzwa zawadi murua
(j) Andika sentensi ifuatayo upya bila kubadilisha maana ukitumia ;hi. (alama 2)
'O'reje Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo. (k) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo: (alama 2)
Wazee watatu walitoka mangweni mchana.
(L) Onesha kishazi huru na tegemezi
Msichana mtukutu alifukuzwa shuleni leo asubuhi. (alama 2)
(m) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. (alama 2)
(i) Nata (kutendesha)

(ii) Kaa (kutendana (alama 3)
(n) Bainisha yambwa katika sentensi ifuatayo.
Mgeni aliandaliwa chakula kitamu na mwenyeji wake kwa sinia. (alama 2)
(o) Tambua matumizi ya kiambishi –ji- e.
Jino la jitu hilo lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiaji yul (p) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana ya vitate *rika* na *lika.* (alama 2) (alama 2)
(q) Tambua aina ya vihusishi katika sentensi zifuatazo.
(i) Jumba lifuatalo li mbele ya msikiti wa Musa. (alama 2)
(ii) Kisiwa cha Giningi kimekauka
(r )Tambua hisia zinazojitokeza katika sentensi hizi:
(i) Ngo! Mtu kama wewe hawezi kufaulu. (alama 2)
(ii) Maskini! Alikuwa moto maskini.
(s) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya nahau ifuatayo.
Zunguka mbuyu (alama 2)
ISIMUJAMII(ALAMA 10) (alama 8)
(a) Eleza dhana ya uwingi lugha.
(b) Fafanua mambo **manne** yanayochangia uwingi lugha katika jamii.

(al.2)

MTIHANI WA 12

a) Onyesha mzizi na kitenzi . (al.2) (al.2)

i) hakimbii ii) hifadhi

b) Ainisha maneno yaliyopigwa mstari.Naam , ameleta machache.

c) Eleza sifa za sauti hizi :-

/e/
/g/
d) kwa kutoa mfano eleza maana ya sentesi changamano. (al.2)

e) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano:- (al.2)
i) wa (tendea)
ii) - fa
(tendesha)

f) Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno "chuma". (al.2)

g) Ainisha viambishi katika kitenzi :- (al.3)
Lililoliwa

h) Eleza maana mbili za sentensi:- (al.2)
Alikuwa amenijuza kuwa angefika kwao.

i) Eleza matumizi ya 'kwa' katika sentensi hii : (al.3)
Kwa nini umeishi kwao kwa muda huu wote?

j) Yakinisha sentensi ifuatayo . (al.1)
Usipoziba ufa utajenga nyumba.

k) Eleza matumizi ya neno lililopigiwa mstari katika sentesi hii:- (al.1)
Alitembea Kitausi kupokea zawadi.

l) Changanua sentesi hii kwa matawi. (al.3)
Mlango umevunjwa na aliyeujenga.

m) Andika katika usemi wa taarifa :- (al.2)
"Hicho kijicho cha paka leo ni marufuku kwangu. " Mzee kazibwe alisema.

n) Andika upya sentensi ifuatayo ukibadili vitenzi vilivyomo kuwa nomino (al. 2)
Mayaka anapotumbuiza huchekesha sana.

o) Unganisha sentensi zifuatazo kuwa sentensi moja bila kurudia kitenzi (al 2) Kimathi amempigia Wanjiru simu. Wanjiru amempigia Kimathi simu.

p) Bainisha virai vilivyopigiwa mstari
<u>Kalamu na karatasi</u> hutumiwa na <u>wasiolala</u> (al 2)

q) Sahihisha sentensi ifuatayo:- (al 1)
Sukari zilizowekwa mfukoni zilinyeshewa

r) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania (al 2)

s) Tumia 'o' kirejeshi tamati (al 1)
Haya ni maongezi ambayo yanafaa

t) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi (al 1)
'mighairi ya'

u) Eleza matumizi mawili ya kamusi (al 2)

<u>ISIMU JAMII (AL 10)</u>

a) Lingua Franka ni nini? (al 2)
b) Fafanua sifa tatu za Lingua Franka (al 3)
c) Lugha mwiko ni lugha gani? (al 1)
d) Kuhamisha msimbo ni nini? (al 1)

e) Eleza sababu zozote tatu zinazochangia kufa kwa lugha (al 3)

## MTIHANI WA 13

(a) Toa mifano miwili miwili ya (al.2)

i. Sauti ghuna ambazo ni vipasuo ……………………………………………..

ii. Sauti sighuna ambazo ni vikwamizo ……………………………………………

(b) Onyehsa mofimu katika neno **Aliyemcha** (al.2)

(c) Andika sentensi yenye muundo ufuatao (al.2)

KN(W+V) + KT (t +RH)

(d) Tumia neno shirika kama nomino na kama kielezi katika kutunga sentensi moja (al.2)

(e) Kwa kutunga sentensi vumisha nomino nguruwe kwa kivumishi cha idadi bainifu. (al.1)

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kutendewa (al.1)

Mtoto wa waziri amekufa

(g) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi (al.2)
Msomi hakutuzwa siku hiyo

(h) Tunga sentensi moja inayobainisha maana mbili tofauti za neno chuma (al.2)

(i) Tambua kiima na aina za yambwa katika sentensi ifuatayo. (al.4)

Mwalimu mkuu hupigiwa nguo pasi na Maria

(j) Kwa kutumia mifano mwafaka fafanua miundo yoyote miwili ya kirai nomino (al.2)

(k) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi (al.2)

Mgeni huyo na mwingine walikula wali kwa uma

(l) Andika neno lenye silabi funge yenye muundo wa konsonanti moja (al.1)

(m) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika udogo wingi (al.2)

Ng’ombe wangu ana ndama mdogo

(n) Tunga sentensi zenye mipangilio ifuatayo; (al.4) i. Kishazi tegemezi na kishazi huru

ii. Kishazi tegemezi na kishazi tegemezi

(o) Eleza matumizi ya ‘ki’ katika sentensi ifuatayo: (al.3)

Nyamunga na kitoto wamekuwa wakila, wakiimba kikasuku

…Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi. (al.4) Mtoto

wa mjomba alikuja kwetu nyumbani jana

(p) Andika kwa msemo wa taarifa. (al.2)

'Yafaa tumwendee mama mkubwa ili atushauri juu ya jambo hili,' Amina alipendekeza.

(q) Andika kinyume cha: (al.1)

Chakula hiki kitamu nitakimeza

(r) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo.

al.2 (i) Kiwakilishi nafsi huru

(ii) Kiwakilishi nafsi kiambata

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza sababu tano zilizochangia katika maenezi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki kabla ya Uhuru.

(al.5)

(b) Eleza hatua tano ambazo zimesaidia kuikuzalugha ya Kiswahili baada ya Uhuru nchini Kenya.

(al. 5

## MTIHANI WA 14

a) (i) Taja konsonati mbili zinazotamkiwa katika kaakaa gumu. (al.2) (ii) Sauti ulizotaja hapo juu ni za aina gani? (al.2)

(b) Shadda ni nini? (al.1)

(i) Weka shadda katika maneno yafuatayo.

(al.2)

Ua

Kiwakilishi

(c) Tunga sentensi mbili kuonyesha dhana tofauti zinazobainishwa na kiimbo.

(al.2)

(d) (i) Kiambishi ni nini? (al.1)

(i) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo. (al.3)

Kilicholiwa.

(e) Bainisha maneno katika sentensi ifuatayo.

(al.3)

Kumbe mtu mfupi anarukia lile zuri.

(f) Maneno yafuatayo yamo katika ngeli gani. (al.2)

(i) Wembe

(ii) Mnyoo

(g) Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa wingi.

Ngamia alibeba hema lililotengenezwa kwa ngozi ya chui. (al.3)

(h) Tunga sentensi inayodhihirisha matumizi ya 'O' rejeshi tamati.

(al.2) (i) Onyesha hali iliyotumika katika sentensi ifuatayo.

(al.1) (i)Mganga aonekana akiwa uchi.

(ii) Kanusha. (al.1)

Ningekuwa kasisi ningewafanya mwende mbinguni.

(j) Eleza matumizi mawili ya kiambishi –ji-

(al.2)

(k) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya visanduku.

(al.4)

Ng'ombe akamuliwaye atachinjwa kesho.

(l) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (al.3)

Mtaalamu alituambia kuwa kusoma kwa mapana kungepalilia ubunifu wa wanafunzi hao wao.

(m) Andika maneno yafuatayo katika kauli ulizopewa mabanoni.

(al.2)

(i) Fumba (tendata)

(ii) Kwaa (tendama)

(n) Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha maana mbili za kitawe 'somo'.

(al.2)

(o) Tambua shamirisho na chagizo katika sentensi hii.

(al.2)

Juma alimjengea nyanya nyumba kwa mawe vizuri sana.

ISIMU JAMII.

a) Eleza istilahi zifuatazo za isimu jamii. (al.4)

(i) Lugha ya taifa.
(ii) Lugha sanifu.
(iii) Lugha rasmi.
(iv) Lahaja.

(b)Fafanua maswali sita yanayochangia kustawi kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (al.6)

## MTIHANI WA 15

a) Andika sifa zozote mbili za sauti zifuatazo.
(alama 2)

i) /u/ ii) /ch/

b) Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike muundo wake.
(alama 2)

i) igwa ii) oa

c) Andika upya sentensi kwa kutumia 'O' rejeshi tamati.
(alama 2)

Gari lililoanguka si lile unalolizungumzia.

d) Unda nomino kutokana na kivumishi kifuatacho.
(alama 1) Tepetevu.

e) Badilisha katika usemi wa taarifa.
(alama 3)
Afisa wa usalama alisema kuwa wangemsaidia ikiwa angeshirikiana nao.

f) Pambanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha Vishale.
(alama 4)
Letu lililopaliliwa limetuletea mazao wengi.

g) Ainisha virai vyovyote vitatu.
(alama 3)
Mwanafunzi yule mtoro hpenda kutembea katikati ya barabara kila wakati.

h) Tunga sentensi moja kutofautisha vitate vifuavyo:
(alama 2)
i) Chaka ii) Shaka

j) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao, hali timilifu.
(alama 2) Mwanafunzi aliandika insha nzuri.

k) Andika sentensi hii katika udogo wingi.
(alama 2)
Mtoto amefunga mlango wa nyumba yao.

l) Onyesha matumizi mawili ya alama ya vifungo katika sentensi.
(alama 2)

m) Eleza maana ya kishazi.
(alama 1)

n) Nyambua vitenzi vifuatavyo kama ulivyoelekezwa.
(alama 2)
i) Suka (kauli ya kutendata)
ii) Pa (kauli ya kutendeka

o) Onyesha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo. Babu alijengewa nyumba kwa mawe na Juma.
(alama 3)

p) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa.
Mzazi alishangilia matokeo ya mwana. (alama 2)
(Anza: Mwana . . . .)

q) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo.
Mama alinileteа Kanga. (alama 2) r) Yakinisha.
Usiponiita sitaandamana nawe. (alama 2) s) Ainisha kitenzi katika sentensi ifuatayo.
(alama 1)
Mgeni amewasili leo.

ISIMU JAMII.

1. Tofautisha kati ya uwili lugha na wingi lugha.
(alama 4)
2. Taja sababu sita zinazosababisha watu kubadili na kuchanganya ndimi.
(alama 6)

## MTIHANI WA 16

a) Eleza tofauti iliopo kati ya sauti /e/ na /u/
(alama 2)

b) Onyesha muundo wa silabi ya kwanza katika maneno yafuatayo. (alama 2)

(i) Ng'arisha

(ii) Nzi

c) Ainisha vipashio vya kisarufi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Amenifia

d) Andika katika kauli yakinishi (alama 2)
Hatakuja tusipomuarifu mapema

e) Geuza katika usemi halisi (alama 3)
Mwanafunzi alishangaa na kusema kuwa hakuamini alipata alama nyingi vile katika insha.

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali (alama 4)
Yule mwandishi aliyeshinda tuzo ni maarufu sana.

g) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo (alama 3)
Mtoto alipikiwa chai na mamake kwa sufuria chafu.

h) Tunga sentensi mbili kubaini matumizi mawili tofauti ya Mkwaju (alama 2)

i) Unda nomino mbili mbili kutokana na vitenzi vifuatavyo
(alama 2)

(i) Jaribu -

(ii) Chuma –

j) Onyesha matumizi ya 'kwa' katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

(i) Ameenda kwa Musa

(ii) Alipata alama saba kwa kumi

k) Nyambua katika kauli zilizo mabanoni
(alama 2)

(i) Tua (Tendama)

(ii) Pwa (Tendeka)

l) Andika katika udogo wingi
(alama 2) Ndovu wa kiafrika ameharibu mboga shambani

m) Tunga sentensi kudhihirisha maana ya maneno yafuatayo (alama 2) Susuwaa
Zuzuwaa

n) Onyesha kijalizo katika sentensi ifuatayo.
(alama 1)

Yeye ni mwizi

o) Bainisha vishazi katika sentenzi ifutayo (alama 2)

Aliyempeleka mjini, amemwajiri kazi

p) Tumia kivumishi –pi pamoja na ngeli ya YA-YA kutunga sentensi (alama 2)

q) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo (alama 2)

Kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma

(Anza kwa) kushuka

r) Ainisha virai. (alama 2)

Mzee alilala kando ya barabara

ISIMUJAMII

**a)** Eleza mambo yaliyochangia katika maenezi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki kabla ya uhuru (alama 5) **b)** Eleza sifa tano za lugha rasmi.

## MTIHANI WA 17

(a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo. (alama 2)

(i) Kiyeyusho cha mdomo

(ii) Irabu ya mbele juu

(iii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini

(iv) Kikwamizo sighuna cha menoni

(b) Onyesha muundo wa silabi katika maneno yafuatayo. (alama 2)

(i) igwa

(ii) mchwa

(c) Ainisha viungo vya kisarufi katika sentensi hii. (alama 2)

Alani

(d) Weka vitenzi katika hali ya kuamrisha kwa wingi. (alama 2)

(i) -nywa

(ii) Tubu

(e) Geuza sentensi hii katika usemi wa taarifa. (alama 3)

"Sitakuja shuleni kesho," mwalimu mkuu akasema, "Nitaenda kuhudhuria mkutano Mombasa."

(f) Kanusha bila kutumia 'amba' (alama 2)

Nitavaa viatu ambavyo ni safi.

(g) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha pekee katika ngeli ya:- (alama 2)

U - U

(h) Andika kwa udogo. (alama 2)

Ng'ombe hao walichinjiwa karibu na mji ule.

(i) **Bainisha miundo miwili ya kirai kivumishi.** (alama 2)

(j) **Andika upya sentensi zifuatazo ukitumia <u>visawe</u> vya maneno yaliyopigiwa mstari.**

(alama 2) (i) Babangu hapendi kunywa <u>pombe</u>

(ii) Mgeni alipofika ukumbini, <u>sherehe</u> zilikuwa zimeanza tayari.

(k) **Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo.**

(alama 2)

Yaya alimpikia mtoto chakula kitamu. (Anza kwa: Chakula ...)

(l) **Tumia neno 'jana' kutungia sentensi kama.** (alama 2)

(i) Nomino (ii) Kielezi

(m) **Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi tofauti ya alama ya kinyota.**

(alama 2)

(n) **Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo.**

(alama 3)

Mwajuma alitumia ufunguo kumfungulia Amina mlango.

(o) **Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyothihirika.**

(alama 2) (p) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi.**

(alama 4) Mama alimtembelea mwanawe aliyekuwa mgonjwa.

(q) **Tunga sentensi kuonyesha jinsi kiambishi -ndi- kinavyoweza kutumiwa pamoja na nomino ifuatayo.**

(alama 2) mapambo

(r) **Fafanua maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii:-**

(alama 2) Alitukimbilia sana

ISIMU JAMII. (ALAMA 10)

(a) Eleza sababu **tano** zinazomfanya mtu kufanya makosa ya matamshi na sarufi katika mazungumzo yake.

(alama 5)

(b) Eleza sababu **tano** zinazowafanya vijana kupenda kutumia misimu katika mawasiliano yao.

(alama 5)

## <u>MTIHANI WA 18</u>

a) i)Eleza maana ya sauti mwambatano. (alama1)

ii) Andika sauti mwambatano mbili zinazotamkiwa kwenye kaakaa laini.

(alama1) b)Taja matumizi mawili ya kiimbo na utoe mfano kwa kila moja.

(alama4)

c)Eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili na kwa kila muundo utoe mfano mwafaka. (alama1)

d)Tumia neno mzee katika sentensi kama :

(alama2) i) kivumishi ii)nomino

e)Yakinisha sentensi hii. (alama2)

Usipoamka mapema hutaniona nikienda.

f)Bainisha mofimu katika neno lifuatalo ; Alitufia. (alama3)

g)Ainisha nomino katika sentensi hii.
(alama2) Kundi la wajenzi lilimjengea Mogaka tangi la kuhifadhia maji.
i) Somo ambalo hupendwa nchini ni Kiswahili.
ii) Ufisadi ambao unachunguzwa umezidi.
i) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama2)
Ingawa Mukora alilima kwa bidii hakuvuna mazao yoyote.
j) Onyesha mazingira matatu ambapo mstari mshazari hutumika. (alama3)
k) Tumia mzizi –w- katika sentensi kama : (alama2)
i) kitenzi kisaidizi. ii) kitenzi kishirikishi
l) Changanua sentensi hii kwa kutumia jedwali . (alama4)
Walioiba waliadhibiwa vikali na raia hao.
m) Tunga sentensi ya wakati uliopita hali timilifu. (alama1)
n) Andika kwa usemi wa taarifa. (alama3)
"Tafadhali, nipe maji ninywe. Nina kiu". Mkimbizi alimwambia.
o) Eleza matumizi ya 'po' katika sentensi ifuatayo. (alama2)
Alipowasili alionyeshwa walipo.
p) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama3)
Hamisi alimwinulia seremala mchanga kwa sepetu.
q) Tofautisha maana. (alama2)
i) Ningekuwa na uwezo ningesafiri kwenda ng'ambo.
ii)Ningalikuwa na uwezo ningalisafiri kwenda ng'ambo.
h) Tumia 'o'rejeshi katika sentensi zifuatazo .
(alama2) **ISIMUJAMII** **(alama10)**

1. Eleza maana ya lugha ya taifa. (alama2)
2. Eleza majukumu manne ya Kiswahili nchini Kenya kama lugha ya taifa. (alama8)

## MTIHANI WA 19

a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo.
Kikwamizo hafifu cha maneni al2)
Sauti mwambatano ghuna ya midomoni.
Irabu ya mbele tandazwa.
Kimadende
b) i) Eleza maana ya mofimu huru. (alama 1)
ii) Toa mifano miwili ya mofimu huru. (alama 1) c)
Ainisha viambishi katika neno .
Walimliza. (alama 3) d) Badilisha kielezi `bidii` kiwe kitenzi kwa kukitungia

sentensi. (alama 2)

e) Tunga sentensi moja ukitumia kivumishi cha nomino. (alama 1 f)

Tunga sentensi kubainisha

i. Kihusishi cha kiwango.
ii. Kihusishi cha a – unganifu. (alama 2)

g) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia kiwakilishi nafsi huru;

Oluoch na Maria mtakula saa ngapi? (alama 1)

h) Tumia viunganishi mwafaka kukamilisha sentensi zifuatazo.

i. wanafunzi watafaulu mtihani -------------------watasoma kwa bidii.
ii. Aliachwa --------------------- nafasi ilikosekana. (2 mks)

i) Tunga sentensi ukitumia nomio katika ngeli ya U – ZI pamoja na kiashiria kisisitizi cha mbali kiasi katika wingi. (alama 2)

j) Andika upya sentensi zifuatazo kwa kutumia maagizo uliyopewa.
(Alama 2)

Ukikesha utasinzia darasani. ( tumia 'ngali')

Niliweza kuufanya mtihani vizuri kwa kuwa nilikuwa nimejitayarisha vizuri. ( anza kwa:kujitayarisha----------------------)

k) Yakinisha sentensi hii katika nafsi ya tatu umoja.

Tusipoonana na wazazi hatutapata pesa. ( alama 2)

l) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi ya ritifaa.
( alama 2

m) Geuza sentensi hizi katika kauli ulizopewa kwenye mabano Mwalimu aliyakataa maoni ya wanafunzi . ( kutendwa) mwema alimuokoa mtoto aliyekuwa ametupwa pipani. (kutendata) ( alama 2) n) i) Tunga sentensi ukitumia kiambishi 'na' kudhihirisha umiliki. ( alama 1) ii)Eleza matumizi mawili ya kiambishi.'ki' ( alama 2)

o) i) Eleza maana ya yambwa. ( alama 1) p)

Ainisha yambwa katika sentensi ifuatayo.

*Juma alilimiwa shamba lake kwa trekta na mjukuu wake.* ( alama 3)

q) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo.

Kijana <u>yule mtoro</u> hupenda kutembea <u>katikati ya barabara</u> <u>kila wakati.</u> ( alama 3) r)

Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya visanduku.

Waliofika mapema walituzwa vyema. ( alama 4) s)

Andika visawe viwili vya neno:

dhukuru ( alama 1)

ISIMUJAMII ( ALAMA 10)

Fafaua jinsi shughuli zifuatazo zitachangia kukua kwa lugha ya Kiswahili na kufaikisha ajenda ya amani na maridhiano nchini Kenya.

i) Vyombo vya habari na mawasiliano. ( alama 2) ii)

Uchapishaji ( alama 2) iii) Dini ( alama 2) iv) Siasa ( alama 2) v) Sanaa na maonyesho ya muziki.

## MTIHANI WA 20

a) Taja sauti zifuatazo
ala 3) i) Kipasuo hafifu cha kaakaa gumu ii) Nazali ya kaakaa gumu
iii) Kikwamizo ghuna cha ufizi

b) Eleza miundo miwili ya nomino za ngeli ya u-i Toa mifano
ala 2)

c) Ainisha vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo
ala 2)

Kambazi angali barabarani na angali anaendesha baiskeli ambayo imechakaa

d) Ainisha katika neno lifuatalo
ala 2)

Afaye

e) Tambua nyakati na hali katika sentensi ifuatayo

Mhazigi atakuwa ameunganisha mifupa iliyovunjika ala 1)

f) Eleza matumizi ya kwa katika sentensi hii

Kwa nini umeishi kwao kwa miaka mingi? ala 3)

g) Toa mfano mmoja wa kitenzi cha asili ya kigeni kisha ukinyambue katika kauli ya kutendesheka ala 1)

h) Tunga sentensi mbili ili kubainisha maana mbili za neno ‘kiwavi’
ala 2)

i) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi tahini
ala 2)

j) Changanua kwa njia ya mishale
ala 4)

Kikulacho ki nguoni mwako

k) Bainisha vishanzi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo
ala 2)

Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano

l) Yakinisha sentensi ifuatayo
ala 2)

Asipofika mapema hatampata

m) Onyesha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo
ala 3)

Mwiti alimbebea mjomba mzigo kwa baiskeli

n) Akifisha sentesi zifuatazo ala 2)


@. BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

l) Mama sokoni ataenda asubuhi kesho ii)
Gazeti la Taifa Leo huandikwa kwa Kiswahili

o) Andika katika usemi halisi ala 3)
Chifu wetu alituambia kuwa watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu

p) Kanusha katika ukubwa ala 3)
Mwizi huyu aliiba kisu na ng'ombe wa mwanamke yule

q) Eleza tofauti iliyo kati ya sentensi hizi ala 2) i)
Tulipofika hotelini tulipewa soda na chupa ii) Tulipofika hotelini tulipewa soda kwa chupa

r) Andika neno lingine lenye maana sawa na; ala 1)
Piku -

ISIMU JAMII

a) Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Toa sababu tano ala 5)

b) ……………..Sote tunajua kwamba ni kudura. Makiwa

i) Tambua sajili iliyotumika katika dondoo hili ii) ala 1)
Eleza sifa nne za sajili hiyo ala 4)

## MTIHANI WA 21

1. Eleza tofauti moja kati ya sauti zifuatazo. (al. 2)
   (a) /b/ na /d/
   (b) /z/ na /s/
2. Andika nomino katika sentensi hii.
   Kuzembea kwake kulimsababishia ukata (al. 2)
3. Mofimu zifuatazo ni za aina gani?
   (i) alitufia
   (ii) lakini (al. 2)
4. Kwa kutumia mifano eleza matumizi ya alama ifuatayo ya uakifishaji.
   Parandesi
5. Tunga sentensi zenye vivumishi vya pekee vya kuonyesha dhana zifuatazo. (al. 2)
   (al. 2)
   (i) Umilikisho
   ii) Kutobagua
6. Bainisha virai viwili katika sentensi hii.
   Mashamba mengi yataandaliwa tena msimu ujao.
7. Changanua kwa kutumia jedwali.
   Nitakapofika shuleni kaka atakuwa ameondoka. (al. 2)
8. Eleza matumizi matatu ya kiambishi 'ji'.
9. Andika katika usemi halisi. (al. 4)
   Nilimwambia rafiki yangu kuwa siku hiyo ningejitahidi hadi nikamilishe kazi hiyo.
10. Fuata maagizo kwenye mabano kuandika upya sentensi hii.
    Mama alimkaripia mtoto mtoro. (anza: kwa kitondo .... ) (al. 3)
11. Tunga sentensi itakayodhihirisha kihusishi cha wakati.
12. Eleza matumizi ya 'kwa' na 'na' katika sentensi hizi. (al. 3)
    (a) Nyumbani kwao ni karibu kutoka
    hapa. b) Tutatembeleana leo jioni.
13. Huku ukitumia mfano, eleza dhana ya kauli ya kutendata. (al. 1)
    (al. 2)
14. Bainisha vishazi katika sentensi hii.
    Mhazili ambaye ni mzembe atapigwa kalamu. (al. 1)
15. Tambua aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo.
    Yule aliyekuwa hapa sio mgeni wetu. (al. 2)
16. Tumia neno **hoi** kama chagizo katika sentensi.
17. Andika katika ukubwa.

Mwanaume aliyekamatwa jana alikuwa gaidi.

18. Unda nomino kutokana na kivumishi **mfariji**.



(al. 2)

@. BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

(al. 2)

(al. 1)

(al. 2)

(al. 1)

19. Kanusha: (al. 2)

Utatuimbia nyimbo tamutamu.

20. Eleza maana mbili za neno 'changa'. (al. 2)

21. Neno '**mbuyu**' liko katika ngeli gani? (al. 1)

SEHEMU D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)

MHUSIKA 1: Nidhamu , Mheshimiwa Sudi. Hili ni onyo dhidi ya tabia hiyo.

MHUSIKA II: Nisamehe Bwana……………………

MHUSIKA I: sasa ninakaribisha swali la tatu. Mheshimiwa Mambo, uliza swali lako.

MHUSIKA III:Ninaomba kufahamishwa ni kwa nini Waziri wa Maji ameshindwa kusambaza huduma za maji katika kijiji cha Walalahoi.

**Maswali**

1. Bainisha sajili ya makala haya. (al. 2)
2. Fafanua sifa za sajili hii. (al. 8)

MTIHANI WA 22

a) Taja sauti yenye sifa zifuatazo.

i) Chini – kati, midomo hutandazika.

(Alama 1) ii) Kikwamizo ghuna cha ufizi

(Alama 1) b) Taja muundo wa silabi ya maneno yafuatayo.

(Alama 2) i) Au ii) Mbwa

c) Tunga sentensi ya neno moja iliyo na;

(Alama 2) i) Kikanushi kiima katika nafsi ya pili.

ii) Mtendwa nafsi ya tatu.

iii) Shina iv) Kauli ya kutendea. v) Kiishio.

d) i) Tunga sentensi **moja** inayoonyesha maana ya maneno yafuatayo. (Alama 2) Pagua

Bagua

ii) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo;

Yule mama aliyeremba nyumba yake aliinjika chungu jikoni.

(Alama 2)

e) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha idadi dhahiri

(Alama 1)

f) Onyesha yambwa tendwa na yambwa tendewa katika: Mama aliwapikia wajenzi uji kwa mwiko

(Alama 2) g) Changanua kwa kielelezo cha visanduku.

Mkoba ambao ulipotea juzi umepatikana.

(ALama 4)

H) Eleza maana tatu zinazowasilishwa na kiambishi kilichopigiwa mstari.

(Alama 3)

<u>A</u>lia

i) Andika vitenzi vinavyotokana na majina haya. (Alama 3)

i) Kifaa ii) Msemo iii) Hasidi

j) Eleza matumizi ya 'po' katika sentensi hii.

Alipofika alimwona pale alipokuwa amelala.

(Alama 2) k) Sahihisha sentensi zifuatazo:

i) Shairi ambalo alilotukariria ni lile ambalo alilotoa katika gazeti.

(Alama 2) ii) Mgeni mwenye anakuja ndiye nilimpea kitabu.

(alama 2) L) Tumia viashiria vya kutilia mkazo katika sentensi zifuatazo.

(Alama 2)

i) Kibogoyo _______________________ ndiye anayehitaji meno ya dhahabu.

ii) Vyakula ____________________ mvipikavyo nyinyi, nasi twavipika.

m) Eleza matumizi mawili ya kibainishi.

(Alama 2)

n) Tofautisha sentensi zifuatazo

(Alama 2)

Ningekuwa na pesa ningenunua nguo nzuri.

Ningalikuwa na pesa ningalinunua nguo nzuri.

o) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao.

(Alama 2)

KN(N) + KT ( T + E) + U + KN (N) + KT(T + E)

P) Andika kwa kutumia usemi wa taarifa.

(Alama 2)

``Mimi siwezi tena zogo, nataka kupumzika,`` Yasmin alimwambia Juma. q) Yakinisha sentensi ifuatayo.

Asipokuita usiitike.

(Alama 1)

## 4. ISIMU JAMII

Hujambo bwana: You look familiar, have we ever met before.... Sijui nilikuona wapi?

a) Bainisha sajili ya makala haya kwa kutoa mifano mitatu kwenye makala.
(alama 2)

b) Fafanua sifa nyingine nne za sajili hii ambazo zingejitokeza katika makala haya.
(Alama 4)

c) Kwa kutumia mifano mwafaka eleza kaida nne za matumizi ya lugha.
(Alama 4)

## MTIHANI WA 23

a) i) Eleza maana ya sauti. ( al 1) ii) Kwa kutoa mifano mwafaka, tofautisha kati ya sauti hafifu na sauti nzito. ( al 2)

b) Andika neno moja lenye silambi funge ambayo ni konsonanti.
( al 1)

c) Tunga sentensi kwa kutumia neno vizuri kama:
( al 3)

Kivumishi

Kihisishi

Kielezi

d) Andika sentensi ifuatayo katika umoja.

a. Tukihifadhi ndizi hizi vyema maeneo haya yatakuwa na vyakula vya kutosha.
( al 2)

e) Andika neno moja lenye mofimu zifuatazo.

a. Nafsi ya pili wingi, hali timilifu, shamirisho, mzizi, kauli tendea, kauli tenda. (al 2)

f) Tunga sentesi kuonyesha matumizi yafuatayo ya neno na:

Kiunganishi

Kihusishi ( al 2)

g) Tunga sentensi yenye kishazi tegemezi kinachoonyesha masharti.

h) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo. i. Ng'ombe huyo ( al 2)

i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. ( al 1

a. Nomino ya jamii, kirai kihusishi, kitenzi kishirikishi kipungufu, kielezi cha nomino.

j) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo. ( al 1)

a. Mwanafunzi huyo alipita kwa vile alisoma kwa bidii. ( al 2)

b.Anza kwa nomino ya kitenzi- jina

k) Tumia kijna cha kiasi kumla kutunga sentensi.

l) Kwa kutumia mifano mwafaka, eleza matumizi ya viakifishi vifuatavyo: i) Kinyota ii) kibainishi

m) Tunga sentensi moja kwa kutumia kiunganishi cha kinyume. ( al 2)

n) Tumia 'labda' katika sentensi kuonyesha

i) Uwezekano ( al 2)

ii) Tashwishi

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielezo cha mishale.

Mama na nyanay walinunuliwa jozi za viatu na baba.

p) Andika sentensi moja kwa kutumia Kitenzi'kimbia' katika kauli ya **kutendana.** ( al 1) (al 2)

q) Onyesha matumizi ya **ni** katika sentensi ifuatayo

Matunda yaliyonunuliwa sokoni ni yetu.

r) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya **husuni** na **huzuni**.

s) Andika kisawe cha neno 'vurumai' ( al 4)

t) Bainisha **chagizo** na **yambwa** katika sentensi ifuatayo: Mwizi alimuua baba yake kwa bastola.

u) Tunga kitenzi kutokana na neno 'karamu'

v) Aina ya sentensi yenye kishazi huru na kishazi tegemezi huitwaje? 1) w) ( al 1)

Nomino ' kwapa' limo katika ngeli gani? ( al 2)

<u>D. ISIMUJAMII ( AL 10)</u>

*Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali.* ( al 1)

A: Jina? B:

Ouma James

A: Umri?

B: Miaka ishirini ( al 1)



 (alama

( al 1)

( al 1)



@. BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

A: Una shida gani

B: Ninaendesha sana. Pia kichwa chaniwanga ajabu. ( Anatiririkwa na machozi)

C: Anachukua stethoskopu na kumpima) Utapata nafuu hivi karibui ukinywa dawa nitakazokupa.

Maswali

1. Tambua rejesta inayorejelewa na Makala haya. ( al 2)
2. Fafanua vitabulishi vine vinavyohusishwa na rejesta hiyo. ( al 8)

## MTIHANI WA 24

(a) Taja sauti zozote **mbili** ghuna zinazotamkiwa midomoni. (Alama 2)

(b) Mbali na kutumiwa katika ving'ong'o, eleza matumizi mengine ya kibainishi. (Alama 1)

(c) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (Alama 2)

*Mahabusu walifyeka nyanja vizuri.*

(d) Kando na muundo U-NY, fafanua miundo mingine mitatu katika ngeli ya U-ZI. (Ala 3) (e) Geuza kitenzi kilichopigwa mstari katika sentensi ifuatayo kiwe katika kauli ya kutendata.

*Mtoto <u>alifumba</u> pesa alizoziokota na kumpelekea mamake.* (Alama 1)

(f) Kibadilishe chagizo cha mahati kwa kile cha wakati katika sentensi ifuatatyo. (Alama 1)

*Mchezaji aliucheza mpira mjini Kisumu.*

(g) Maneno yaliyopigwa mstari ni kirai kitenzi. Eleza muundo wake. (Alama 3)

*Wao <u>wamezoea kuwamba ngoma</u>.*

(h) Geuza sentensi ifuatayo katika ukubwa. (Alama 2)

*Ng'ombe yule amegongwa na gari.*

(i) Andika sentensi hii upya kwa kutumia kinyume cha kitenzi kilichopo. (Alama 2)

*Wageni waliabiri ndege.*

(j) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi. (Alama 4)

*Mwanafunzi yule ni shujaa kwa sababu amepasi mtihani wake.*

(k) Eleza vipashio vidogo vya kisarufi katika neno lifuatalo. (Alama 3)

*Walisameheana*

(l) Mbali na kirejeshi *amba-* na *o-rejeshi*, tunga sentensi ingine katika ngeli ya A-WA kwa kutumia kirejeshi. (Alama 2)

(m) Tumia neno lililo kwenye mabano kama kielezi. (Alama 1)

*Wanafunzi walishirikiana (Ndugu)*

(n) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo. (Alama 2)

*Walikaribishwa na mwalimu.*

(o) Mbali na kutumika kuonyesha kauli, eleza dhima zingine mbili za viambishi tamati(Alama 2)

(p) Tunga sentensi moja yenye vishazi viwili tegemezi. (Alama 2)

(q) Herufi kubwa hutumika mwanzoni mwa sentensi na nomino za pekee. Eleza matumizi yake mengine matatu kando na haya. (Alama 3)

(r) Andika katika usemi wa taarifa. (Alama 3)

*"La! Mtoto amegongwa vibaya!"Baba alisema.*

(s) Tunga senteni moja itakayodhihirisha maana tofauti ya maneno yafuatayo. (Alama 2)

(i) Changa

(ii) Janga

ISIMU JAMII

(a) Eleza istilahi zifuatazo (Alama 4)

i) lugha ii) misimu

(b) Andika sifa zozote sita za lugha utakayotumia kuwatangazia watu kinyang'anyiro cha soka. (Alama 6)

## MTIHANI WA 25

(a) Taja sauti zifuatazo

(i) Kikwamizo sighuna cha ufizi (alama 1)

(ii) Nusu irabu ya kaakaa gumu (alama1)

(b) kwa kutoa mifano eleza tofauti kati ya silabi wazi na silabi funge. (alama2)

(c) Bainisha mofimu katika neno:

Atamnywea (alama3)

(d) Ainisha vitenzi katika sentensi hii (alama1)

Wanafunzi walikuwa wanakariri mashairi

(e) (i) Eleza maana ya ngeli. (alama1)

(ii) Neno tembo linaweza kuwekwa katika ngeli mbili tofauti zitaje. (alama2)

(f) Andika katika hali ya ukubwa wingi (alama2)

Mzee huyu ana wake wengi.

(g) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama2)

Hawakuwa wakicheza wala kuimba.

(h) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. (alama1)

Tabasamu alijenga nyumba ya babu.

(i) Tunga sentensi moja yenye masharti yasiyowezekana . (alama1)

(j) Andika katika msemo wa taarifa. (alama 2)

"Nimeenda kumtembelea nyanyangu. Hatujaonana tangu mwezi jana," mjukuu alisema

(k) Kwa kutoa mifano eleza matumizi mawili tofautiya alama ya vifungo. (alama 2)

(l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (alama 4)

KN(N+ S) +KT(T+KH+KE)

(m) Tumia ni katika sentensi moja kuleta dhana ya kitenzi na kielezi. (alama 3)

(n) Onyesha aina za shamirishokatika sentensi ifuatayo (alama 3)

Watoto wanalipiwa karo kwa hundi na wazazi wao

(o) Eleza maana mbili za sentensi hii

(alama 2 )

Njoki amkimbilia Fatuma

(p) Tunga sentensi mbili kutofautisha vitate hivi kimaana
(alama 2)

Landa

Randa

(q) Tumia kirejeshi 'o' tamati katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Cheo ambacho amepewa ni kile ambacho anakitaka.

(r) Iandike sentensi upya kulinga na maagizo (alama 2)

Mwanariadha mmoja tu ndiye aliyefuzu katika mbio hizo (Tumia hakuna na ila)

(s) (i) Eleza maana ya shadda.
(alama 1)

(t) (ii ) Weka shadda katika maneno yafuatayo.
(alama1)

Mahakamani

Nchi

ISIMU JAMII (Alama 10)

(a) Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha lugha ya Kiswahili
(alama 5)

(b) "….watu wa kaunti ya makueni wamesahaulika kabisa. Ningependa kuelezwa kinagaubaga kama hawa ni wakaenya au la. Order! Order! Mheshimiwa Tata.

La! Tumekuwa marginalized kwa muda mrefu sana……

(i) Hii ni sajili gani? (Alama 2)

(ii) Eleza sifa tatu za sajili iliyotajwa. (Alama3)

MTIHANI WA 26

a. Eleza kwa kutoa mifano tofauti kati ya ala tuli na ala sogezi. (Alama2)

b. Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo. (Alama 3)

i. Nafsi ya tatu umoja ii. Wakati uliopita iii. 'O' Rejeshi iv. Kitendwa v. Mzizi vi. kiishio

c. Tunga sentensi yenye muundo ufuatao : (alama.2) KN (N) + KT (T + E) + U + KN (N) + KT(T +E)

d. Unda nomino mojamoja kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama.1)

i. Jaribu

ii. Chuma

e. Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi (alama.2)

Usingeacha masomo,usingetaabika vile

f. Onyesha aina mbili ya vishazi kwenye sentensi ifuatayo. (alama.2 Tulibeba maji ya kutosha tulipoenda safari Turkana. g. Akifisha sentensi ifuatayo ipasavyo. (alama.2

Juma maria ulimwona Farida Maria la hakuwepo jana

h. Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi la katika kauli ya kutendwa. (alama.2

i. Andika kwa ukubwa –wingi (alama.2 Ndivu wa kiafrika ameharibu kichaka

j. Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi (alama.2
Ruheni alishauriwa na kasisi aache tabia ya ulevi

k. Tunga sentensi moja itakayodhihirisha maana ya maneno haya mawili (alama.2
Shombo
Chombo

l. Neno 'tikiti'hupatikana katika ngeli mbili tofauti.Taja ngeli hizo na utunge sentensi kwa kila moja
(alama.3

m. Kanusha sentensi ifuatayo (alama.2 Jamila akiimba vizuri atapewa zawadi

n. Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi (alama.2
Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo.

o. Ainisha virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo (alama.3
Mtoto Yule mtukutu hupenda kucheza katikati ya barabara kila wakati. p. Eleza matumizi ya KU katika sentensi.
Sikumwelewa alivyoeleza namna ya kuwatunza mbwa wake
(alama.1 q. Tumia mzizi – enye katika sentensi kama; (alama.2
i. kihusishi ii
.kiwakilishi

r. Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa . Mama alishangilia arusi ya mwana (alama.1
Anza: Arusi….

s. Sahihisha sentensi ifuatayo
Mwanafunzi ambaye aliyepita mtihani amefuzwa
(alama.1 t. Changanua sentensi ifuatayo kwa visanduku
(alama.3 Ule mkongojo ulioletwa na babu utauzwa na fundi maarufu

ISIMUJAMII

1. Taja na ufafanue nadharia tatu zinazoelezea asili ya lugha ya Kiswahili (alama 6 2. Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimujamii
(a) Lafudhi
(Alama 2)
(b) Rejesta
(Alama 2)

## MTIHANI WA 27

a. Toa mfano mmoja mmoja…………wa sauti zifuatazo (Al.2)
(i) Kipasuo ghuna cha ufizi.
(ii) Kiyeyusho cha midomo.
(iii) Irabu ya nyuma juu, mviringo
(iv) Sauti mwambatano inayotamkiwa kwenye ufizi

b. (i) Eleza maana ya silabi (Al.1)
(ii) Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi (Al.1)
KKKI + KI

c. Ainisha matumizi ya kiambishi na katika sentensi ifuatayo.
Nina na Tina wanasaidiana na Dina

d. Badilisha nomino zilizopigiwa msitari kuwa vielezi katika sentensi. (A.2)
i) Mashujaa wa kijeshi walipigana hadi wakashinda
ii) Wakoloni walitawala Kenya hadi mwaka wa 1963.

e. Tunga sentensi ukitumia kihusisha cha kiwango (Al.2)

f. i) Eleza maana ya kirai (Al.2) ii) Ainisha virai vilivyopigiwa msitari. (Al.1)
Zana hizi zimeundwa na mafundi wenye ustadi mkubwa.

g. Tambulisha miundo miwili ya nomino za ngeli ya Ki-Vi. (Al.2)

h. Tunga sentensi ukitumia wakati uliopita hali timilifu. (Al.1)

i. Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika hali ya udogo wingi. (Al.2) Buzi lili hili lilikula mmea wa janajike lile.

j. Bainisha maana tatu zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo. (Al.3)
Alininuliwa ng'ombe na mtoto wake

k. Tunga sentensi mbili kuonyesha maana mbili za neno Ila. (Al.2)

l. Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (Al.2)
Wakili alimtahadharisha mshukiwa kwamba asingemwarifu ukweli wote kuhusu kesi hiyo asingemwakilisha.

m. Changanua sentensi hii kwa kutumia kielelezo cha matawi.
Mwalimu Yule alimwadhibu mwanafunzi aliyekuwa amechelewa.
(Al.4) n. Ainisha yambwe katika sentensi ifuatayo (Al.3) Baba alipikiwa chai na yaya kwa sufuria.

o. Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya vifungo. (Al.2)

p. Andika sentensi hii kwa kinyume (Al.1)
Furaha amehama mjini

q. Andika sentensi ifuatayo upya kulingana na maagizo. (Al.2)
Wachezaji hawakucheza mpira kwa sababu ya mvua. (Anza kwa: Mpira …………….. r. Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo(Al.2)
Viwanda vikianzishwa mashambani idadi ya wanaohamia mjini itapunguzwa. s. Amrisha katika wingi. (Al.1) Amka.

C. ISIMUJAMII (AL. 10)

Eleza sifa zozote tano za lugha ya siasa

MTIHANI WA 28

(a) Ziandike sentensi zifuatazo ukitumia kiwakilishi cha pekee o-ote. (alama 2)

(i) Ufunguo wowote ufunguao ni wetu.

(ii) Ngozi zozote zirarukazo ni za kifaru.

(b) Taja sauti zozote *nne* zinazotamkiwa katika ufizi. (alama 2)

(c) Andika sentensi inayoonyesha 'ki' ya masharti. (alama 1)

(d) Onyesha viambishi awali na tamati katika kitenzi: Alimkemea. (alama 1)

(e) Bainisha matumizi ya 'ni' katika senntens zifuatazo. (alama 2)

(i) Ondokeni.

(ii) Kiptoo ni mwizi sugu (alama 2)

(f) Eleza maana *nne* zinazojitokeza katika sentensi hii.
(i) Alimpigia simu (alama 2)

(g) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi.
(i) Vile vingali vikitengenezwa (alama 3)

(h) Akifisha sentensi ifuatayo. (alama 2)
(i) Puka chaka hata wewe siamini.
(i) Eleza tofauti kati ya sentensi hizi mbili.
(i) Ungesoma kwa bidii ungepasi mtihani. (alama 2)
(ii) Ungalisoma kwa bidii ungalipasi mtihani. (alama 1)
(j) Andika sentensi moja kwa kutumia 'licha ya'. (alama 3)
(k) Andika ukubwa na udogo wa neno rununu.
(l) Andika sentensi zifuatazo kwa wingi.
(i) Domo limepinduliwa.
(ii) Kiwiko kimejigonga ukutani. (alama 2)
(iii) Ukimwi umeangamiza wengi duniani.
(m) Unda vivumishi kutokana na maneno yafuatayo.
(i) Imani
(ii) Ubora (alama 2)

(n) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendesha.
(i) – nya (alama 2)
(ii) - cha (alama 2)
(o) Taja maana *mbili* ya neno 'mjomba'.
(p) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)
"Ala! Huna heshima wewe mtoto!"
Mama alimkaripia bintiye:
(q) Kamilisha methali zifuatazo. (alama 3)
(i) Ukuni juu ya uchaga
(ii) Simbiko haisimbuki ila
(r) Eleza maana ya misemo ifuatayo.
(i) Msumari wa moto juu ya kidonda. (alama 3)
(ii) Pasulia mbarika.
(iii) Giza la ukata.
(s) Onyesha kirai nomino, kirai kivumishi na kirai kielezi katika sentensi.
(i) Bawabu mzuri huandika ripoti ndefu mara kwa mara.

4. ISIMU - JAMII

(a) Eleza ukionyesha bayana tofauti baina ya lahaja na lafudhi. (alama 4)
(b) Taja sifa tambulizi za lugha ya misimu (alama 3)
(c) Orodhesha sifa kuu za sajili ya siasa. (alama 3)

## MTIHANI WA 29

(a) Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo (al.2) i. Kikwamizo sighuna cha ufizi
ii. Irabu ya mbele juu tandazwa

(b) Tambua mofimu katika sentensi ifuatayo (al.3)
Awaibiaye

(c) Eleza matumizi ya kiambishi 'ni' katika sentensi ifuatayo (al.2)
Halima ambaye ni rafiki yangu tangu utotoni, alinitembelea nyumbani juzi.

(d) Tumia nomino 'sherehe' kama kitenzi katika sentensi (al.2)

(e) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mambano (al.2) i. Tua(tendama
ii. Fumba(tendata

(f) Tumia kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi kutunga sentensi. (al.2) (g) Bainisha aina za nomino katika sentensi hii (al.2)
Kucheka kwa bwana Omari kulionyesha raha baada ya kuionja asali.

(h) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari. (al.3)
Ukeketaji wa wasichana umepingwa na jamii yenye msimamo imara.

(i) Tunga sentensi moja yenye kuonyesha aina tatu za shamirisho (al.3)

(j) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi (al.2)
Usiposoma kwa bidii, hutapita mtihani.

(k) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu (al.2)
Mhubiri huwasomea waumini kitabu kitakatifu.

(l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (al.3)
KN(N+V+E)+KT(T+H+N)

(m) Tunga sentensi kubainisha kivumishi cha pekee chenye maana ya 'bila kubakiza' (al.1)
Andika sentensi ifuatayo kwa wingi (al.2)
Kilema mwingine alikuja kwangu.

(n) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi (al.4)
Simba waliojeruhiwa jana walikimbia vichakani.

(o) Andika kwa usemi halisi (al.2)
Njoroge alisema alikuwa amepata alama zote katika mjarabu wa siku iliyotangulia.

(p) Andika sentensi ifuatayo ukitumia kinyume: (al.1)
Mama yule mfupi alianika nguo za mwanawe.

(q) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa (al.2)
Mtoto wa mzee yule aligongwa na nyundo alipofukuzwa na mbwa.

4.ISIMU JAMII (al.10) “Nataka

(a) Tambua sajili inayorejelewa na kifungu hiki. (al. 2)

MTIHANI WA 30

a) Eleza sifa mbili mbili za sauti hizi. (alama 2)
/i/
/ch/

b) Huku ukitoa mifano tofautisha ala sogezi na ala tuli. (alama 2)

c) **Yakinisha.** (alama 1)
Mamlaka makubwa ya Rais hayakwazi juhudi za upinzani.

d) Huku ukitoa mifano, tofautisha silabi funge na silabi wazi. (alama 2)

e) Tia shadda katika neno lifuatalo ili litoe maana mbili tofauti. (alama 2)
Walakini

f) **Andika katika usemi wa taarifa.** (alama 2)
“Nitawafuta kazi wafanyikazi wote wanaozembea kazini.” Waziri aliwaonya.

g) Tunga sentensi moja ukitumia nomino katika ngeli ya U - YA. (alama 2)

h) Tumia kitenzi –fa katika sentensi sahihi kuonyesha kauli ya kutendesha. (alama 1)

i) Tambua kiima na yambwa katika sentensi hii. (alama 2)
Mwanafunzi alipewa zawadi na mwalimu mkuu.

j) Tambua na ueleze hali na nyakati katika sentensi hii. (alama 2)
Sehemu hii yampendeza mtu ambaye anapenda kutalii.

k) Changanua kwa njia ya jedwali. (alama 3)

kuunga mkono mbunge mwenzangu katika mswada huu wa kupiga marufuku unywaji wa pombe hii haramu… Bwana Spika….”

Wanafunzi wengi waliosoma kwa bidii hawakuathirika na udanganyifu wa mitihani.

l) Bainisha maana mbili zinazotokana na sentensi hii. (alama

2) Wanafunzi walisomeana barua.

m) Tumia chagizo ya idadi badala ya uliyopewa katika sentensi ifuatayo. (alama

2) Tulimtembelea nyanya Jumamosi iliyopita.

n) Bainisha matumizi ya kiambishi KU katika sentensi hii. (alama

3) Mkurugenzi hakukusaidia ulipoenda kule Mombasa anakofanya kazi.

o) Andika Methali inayojumuisha ujumbe ufuatao. (alama 2)
Hata mtaalamu huhitaji kutafuta msaada wa wataalamu wenzake.

p) Bumba ni kwa nyuki ………………………. ni kwa samaki na ……………………… ni kwa siafu.
(alama 2) q) Tunga

sentensi moja kutofautisha kimaana jozi lifuatalo. (alama 2) Pure

Bure

Tunga sentensi moja kuonyesha maana mbili za neno: *Mradi*. (alama 2)

r) Taja dhana zinazowakilishwa na Mofimu zilizopigiwa mstari. (alama 2)

Some**ni**

**U**kuta

s) Unda majina mawili kutokana na neno **dhuru**. (alama 2)

ISIMUJAMII (Alama 10)

a) i) Eleza dhana ya misimu. (alama 1)

ii) Taja sifa nne za misimu. (alama 4)

b) i) Eleza maana ya lakabu. (alama 1)

(ii) Eleza dhima ya lakabu katika jamii. (alama 4)

Mshtakiwa alidai kwamba alikuwa ameonewa kwa kuwa hakuwa ameshiriki ulevi kutoka mwaka uliokuwa

## MTIHANI WA 31

(a) **Badilisha sentensi ifuatayo iwe mazoea kwa kutumia kirejeshi "O"**

Mtoto anayelia huchapwa

(b) **Andika kinyume**

Wavulana watatu wanaingia darasani kwa haraka.

(c) **Andika sentensi tatu ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii:-**

Kule ndimo alipoingia

(d) **Taja aina za vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi iuatayo**

Mama amewahi kupika jikoni

(e) **Eleza maana ya misemo ifuatayo** :-

(i) Giza la ukata…

(ii) Meza mate machungu

(f) **Unda vitenzi kutokana na** :-

(i) Mkufunzi

(ii) Maeneo

(g) **Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, taja aina za sentensi za kiswahili**

(h) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vishale**

Mwalimu huyu mzuri anafundisha darasani.

(i) **Eleza maana mbili za sentensi** :-

Mama alimlimia mwanawe shamba

(j) **Akifisha sentensi ifuatayo**:-

ah huu ndio upuuzi aliotuitia mmoja wao akaropoka.

(k) **Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano**

(l) **Andika sentensi ifuatayo katika msemo halisi** :-

umetangulia.

(m) **Pambanua viungo vya kisarufi katika kitenzi kifuatacho**

Tuliwalimia

(n) **Andika upya sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo:**

Mizizi ya mibaruti hii iliwaponya watu ambao walikuwa na shida kama hii yenu (**kanusha kwa umoja**)

(o) **Tunga sentensi ukitumia neno "Vile" kama:**

(i) Kiwakilishi
(ii) Kivumishi
(iii) Kielezi

(p) **Bainisha matumizi viambishi "ku" na "Ji" katika sentensi zifuatazo:-**

(i) Mwanafunzi hukusoma kwa bidii
(ii) Atakupiga
(iii) Amejikata
(iv) Mchezaji huyu ni hodari

(q) **Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa huku ukikanusha**

Kijibwa changu ni kikali sana

## MTIHANI WA 32

(a) **Jaza mapengo:-**

| **Kutenda** | **Kutendesha** |
|---|---|
| (i) Chota | |
| (ii) Lewa | |

(b) **Taja sauti moja ya;**

(i) King'ong'o
(ii) Kiyeyusho

(c) **Tumia neno "*shujaa*" katika sentensi kama:-**

(i) Kivumishi
(ii) Kielezi...

(d) **Tambua vitenzi katika sentensi hii kwa kuvipigia mistari:-**

Sisi tulikwisha kutambua alikuwa na nia mbaya. Yeye ndiye mwizi .

(e) **Andika wingi wa sentensi hii katika hali ya ukubwa:-**

Kichinjio hiki kilikarabatiwa kwa pesa nyingi

(f) **Eleza maana zinazojitokeza katika vifungu vifuatavyo:-**

(i) Jambazi kutoka dukani liliiba.
(ii) Liliiba jambazi kutoka dukani.
(iii) Kutoka dukani jambazi liliiba.
(iv) Jambazi liliiba kutoka dukani.



@. BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

(g) **Jaza neno ambalo ni kinyume cha lile lililopigwa mstari katika sentensi:-**

(i) Vile vitu <u>ulivyovichanganya</u> itakubidi

(ii) Bomba hili l<u>imeziba</u> mwite fundi aweze

(h) **Unganisha sentensi hii kwa kutumia *'O'* rejeshi :-**

Wavu umekatika. Wavu ni wao

(i) **Eleza matumizi mawili ya "*ka*" na utunge sentensi kwa kila mojawapo**

(j) **Yakinisha sentensi hii:**

Sijafahamu kwa nini hawamkaribishi mpwa wao.

(k) **Andika katika usemi halisi:-**

Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo

(l) **Akifisha sentensi ifuatayo:-**

Sijaona kitabu kizuri kama mayai waziri wa maradhi, utaniazima siku ngapi bashiri alimwuliza rita

(m) **Changnanua kwa njia ya mishale**

Mama anapika na baba akisoma gazeti

(n) **Tunga sentensi moja na uonyeshe kwa mstari;**

(i) Shamirisho kipozi

(ii) Shamirisho kitondo

(iii) Shamirisho ala/kitumizi

(o) **Tungia vitenzi vifuatavyo sentensi katika hali zilizobanwa:-**

(i) Fa(**mazoea**)

(ii)La(**kutendeka**)

(iii) Pa (**kutendea**)

(p) **Tambulisha kishazi tegemezi na kishazi huru**

Wanafunzi walifoanya vyema walituzwa jana

(q) **Pambanua viambishi mbalimbali katika sentensi ifuatayo**

Waliwapendezea

<u>MTIHANI WA 33</u>

a) **Onyesha viwakilishi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani:-**

i) Unamjua vyema kweli? (ii) Hicho wanachokitaka hakipo

(b) **Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi:-**

(i) Minghairi ya

(ii) Wala

(c) **Yakinisha sentensi ifuatayo:-**

Chakula hakipikiki vizuri

(d) **Jibu kulingana na maagizo kwenye mabano:-**

(i) Hatujui ambako alitorokea (**tumia 'O' rejeshi**)

(ii) Angekuwa na pete, angekupatia (**ibadilishe katika wingi kisha uikanishe**)

(e) Bainisha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo:-

Maksuudi alimjengea Tamima Kasri kwa matofali mazuri

(f) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale/mistari:-

Watoto wote wameamka mapema na wazazi wanatayarisha staftahi

(g) Unda nomino moja moja kwa kila kitenzi

Shuku

Vumilia shona lia



@. BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

(h) **Eleza maana ya '<u>jinsi</u>' kama inavyojitokeza katika sentensi zifuatazo**
(i) Naomba unionyeshe jinsi ya kuendesha gari
(ii) Wakenya hawapendezwi na jinsi viongozi wanavyoendeleza ufisadi
(i) **Bainisha aina za nomino zilizopigiwa mistari katika sentensi hii:-**
<u>Uhodari</u> wa <u>wanariadha</u> wa <u>Kenya</u> unahitajika kote duniani
(j) **Tunga sentensi ukitumia mzizi – choyo kama :-**
(i) nomino
(ii) Kivumishi
(iii) Kiwakilishi
(k) **Eleza matumizi <u>mawili</u> ya kila mojawapo wa alama za uakifishaji zifuatazo:-**
(i) msitari
(ii) Parandesi
(l) **Geuza zentensi zifuatazo katika kauli kwenye mabano:-**
(i) Fundi ameharibu saa (**kutendea)**
(ii) Umemwona mgeni? (**kutendewa**)
(m) **Andika kwa udogo:-**
Gari la Mzee Maritu limegonga ng'ombe wa jirani wake

<u>MTIHANI WA 34</u>
(a) *Andika sifa bainifu za sauti*
(i) e:-
(ii) n:-

(b) *Eleza maana ya :-*
(i) Kiimbo:.
(ii) Shadda…

(c) *Tunga sentensi moja moja kudhihirisha ngeli zifuatazo*:-
(i) U-U
(ii) Pokomo /Pa-ku-mu
(d) *Unda kitenzi kimoja kutokana na nomino* 'Mtubia"
(c) Eleza matumizi mawili ya kiambishi '*ku*'
(f) Tunga sentensi ya maneno manne ambayo ina sehemu zifuatazo. Kielezi cha namna,
kivumishi,kitenzi na jina
*Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi*:- (g)


Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

Ng’ombe aliyeletwa juzi ameuzwa leo jioni.

(h) *Onyesha matumizi mawili mawili ya alama zifuatazo:-*

(a) Alama ya mshangao

(b) Mshazari

(i) Tunga sentensi sahihi ukitumia –*wa*- katika kauli ya kutendeana

(j) *Andika udogo wa sentensi:-*

*40*

@. BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

Ndama wa ng'ombe yule ameuzwa.

(k) *Onyesha tofauti ya vitate vifuatavyo kwakuvitungia sentensi*

(i) Dhamani

(ii) Thamani

(l) *Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi*

Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari

(m) *Ainisha shamirisho /yambwa katika sentensi ifuatayo*:-

Mchezaji alimpigia mwenzake mpira kwa mguu wa kushoto.

(n) Huku ukitumia mifano mwafaka, eleza tofauti ya sentensi sahili na ambatano

(o) *Onyesha aina za viambishi katika sentensi hii*:

Nitajisomea

(p) *Andika katika usemi wa taarifa:-*

Tutaanza mashindano kesho, Mwalimu alimwambia mwanafunzi.

(q) *Eleza maana mbili ya sentensi*:-

Tumetengeneza barabara

(r) *Tumia mifano mwafaka kueleza aina za mofimu*

MTIHANI WA 35

a) Unda nomino za/lm,k, dhahania kutokana na maneno yafuatayo :-

i) Kwea .

ii) Himarisha …

b) Huku ukitoa mifano eleza miundo mitatu ya silabi za Kiswahili

c) Tunga sentensi ukitumia kinyume cha kitenzi: 'umba'

d) Andika katika

Meza ii hii ndiyo aliyotumia kulia

e) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendewa

i) cha … ii) nywa

f) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo:

atakuajiri

g) Sisi tunajua sheria ingawa tu wafisadi

Anza: Japo………… h)

Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo:-

i) Wanafunzi wote wameingia darasani

ii) Jaribu kujitahidi kisabuni usianguke mtihani i)

**Changanua sentensi ifuatayo ukitumia njia ya matawi** :-

Amekuja kuwatembelea manusura waliopata ajali ya ndege

j) Taja sifa mbalimbali za sauti zifuatazo:

/Z/

/K/

k) Huku ukitumia mifano ya sentensi eleza matumizi **mawili** ya kiambishi, **'ji'**

l) **Andika udogo wa:**

Magari yote yaliyobakia yatauzwa na mzee yule mwembamba

m) **Sahihisha:**

i) Kila mwanafunzi alipewa ndazi na mayai moja

ii) Nipee huo mkoba nitoemo vitabu zangu

n) **Tumia – 'ako' katika sentensi kama**:

i) Kivumishi ii) Kiwakilishi iii) Kitenzi

o) Bainisha aina **mbili** za vishazi katika sentensi hii :-

Shamba lile kubwa litauzwa kesho

p) **Andika katika usemi wa taarifa** :

"Karibu Rahma, tafadhali kaa," Musa akasema . Ahsante, je, habari za hapa?' Rahma aliuliza q) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi tofauti ya neno: '**somo'**

## MTIHANI WA 36

(a) Taja sauti **mbili** ambazo hutamkwa nyuma ya ulimi kati ya hizi

/h/,/o/,/y/,/u/,/kh/,/g/,

(b) Ng'oa kisiki hiki haraka askari akaamrisha mahabusu

(**Andika kwa msemo halisi**)

(c) **Badili sentensi zifuatazo katika kauli iliyoonyeshwa kwenye mabano**

(i) Si vizuri mwanafunzi kumwibia mwenzake pesa (**Kutendeana**)

(ii) Mpishi aliharibu mchuzi huu kwa kuongeza chumvi nyingi. (**tendeka**)

(d) **Bainisha matumizi ya "po" katika sentensi ifuatayo**:-

Alipowasili alionyeshwa walipo.

(e) **Andika kwa usemi wa taarifa:-**

"Wasichana wakielimishwa wataweza kuwa bora kuliko wavulana," Naibu wa Chansela wa chuo Kikuu aliwaambia mahafala.

(f) **Tunga sentensi ambayo ina aina za maneno uliyopewa:-**

N + V + V + T

(g) **Tumia ''O'' rejeshi ya kati**

Lisemwalo silo liwalo



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

(h) 'Msipokuwa wenye bidii hamtayapata mafanikio maishani.' Yakinisha katika umoja

(i) Changanua kwa kutumia mishale

'Mimi sikumwona wala Mwenda hakumwona'

(j) Tunga sentensi ukitumia maneno haya katika kinyume.:-

(a) afikiana

(b) sifu

(k) Unda nomino mbili mbili kutokana na vitenzi vifuatavyo:-

(i) abudu

(ii) fisidi

(l) Andika katika hali ya ukubwa

Mwanamke huyu amezaa watoto wanne.

(m) Bainisha matumizi ya maneno yaliyopigwa mstari

(i) Mbio hizi hazitakufikisha mbali

(ii) Mwambie Abedi asifanye mbio kuhusu hiyo kazi.

(n) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi

Msichana aliyeitwa alikuwa mkorofi

(o) Eleza dhana zinazowakilishwa na viambishi awali katika sentensi zifuatazo: -

(i) Aliitwa

(ii) Hakupata

(p) Tunga sentensi mbili kubainisha maana tofauti ya maneno yafuatayo:-

(i) Kuna

(ii) guna

(q) Taja mianzo mitatu tofauti ya ngeli ya U-ZI

(r) Eleza maana ya semi hizi :

(i) Kunja jamvi

(ii) Piga kambi

## MTIHANI WA 37

(a) *Andika sentensi ifuatayo bila kutumia* "amba":-

(i) Jitu ambalo linatusumbua sharti liadhibiwe vikali

(ii) *Weka sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea*:-

Mmea ambao unapandwa katika msimu wa masika unamea

(b) *Badilisha sentensi hizi hadi usemi wa taarifa:-*

(i) "Nitarudi tu ikiwa mtakubali kuomba msamaha". Juma alisema

(ii) "Elezeni vile mlivyokuja hapa na namna mtakavyokwenda." Mwalimu mkuu alisema *(c) Fuata maagizo uliyopewa baada ya kila sentensi ili kujibu maswali haya :*



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

(i) Aliogopa kumwangalia simba aliyekula mzoga. (Tumia neno 'Ogofya' bila ya kubadililsha ya sentensi:-)

(ii) Mti wa zambarau ni rahisi kukatwa ukiwa unatumia msumeno. (*Anza* Ni rahisi...)

(d) **Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii** :-

Alimlilia mwanawe

(e) (i) **Kanusha sentensi hii:-**

Tungewalaki kama tungejua watakuja

(ii) **Sahihisha sentensi ifuatayo na uiweke katika wingi**:-

Ningalifanya kazi ningekuwa tajiri

(f) Tunga sentensi **nne** kuonyesha matumizi na maana nne za kijineno **'ki'**

(g) **Tumia kivumishi kilichoko kwenye mabano kukamilisha sentensi:-**

(i) Bibi yule alinunua gari ______________________(-pya)

(ii) Mti (-ingine) ______________________uliangushwa badala ya ule wa kwanza.

(h) **Unda majina mawili mawili kutoka vitenzi hivi na utumie katika sentensi ili kubainisha maana** (i) Safiri (ii) Zaa

(i) **Akifisha kifungu hiki**:-

Yohana na Emanueli walifunga safari wakielekea mashariki kusini na hatimaye magharibi walifikia huko novemba mwaka jana walipokuwa wakirudi walimkuta mwalimu mkuu njiani ambaye alishtuka kuwaona pale

(j) ***Geuza sentensi hii hadi udogo***:-

Nyoka yule mrefu alifukuzwa na watu wengi

(k) ***Andika upya sentensi hii kwa kuandika kinyume cha kila neno lilipigwa mstari***:-

Wifi <u>alipovaa</u> nguo na kusimama ajuza yule <u>alikaa</u>

(l) Sauti hizi ni za aina gani na hutamkwa wapi?

(i) **gh**

(ii) **j**

(m) Mahabusu walifyeka uwanja vizuri

**Andika sentensi hiyo upya ukimaliza kwa neno mahabusu**

## <u>MTIHANI WA 38</u>

(a) **Onyesha maneno yaliyokopwa toka lugha za kigeni na kuswahilishwa kwa kuyaongezea irabu** ***k.m. Bint (Kiarabu) – Binti***

Toa mifano minne

(b) *Andika sentensi ifuatayo kwa usemi halisi:*

Mwalimu alipoingia darasani aliuliza kitabu chake kilipokuwa.

(c) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi nafsi huru umoja

(d) **Kanusha sentensi hizi kwa wingi**:-

(i) Mtoto huenda shuleni kila siku



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

(ii) Mwalimu amemfunza mwanafunzi vizuri

(e) **Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo**

Wanafunzi waliandikiana barua

(f) **Ziandike sentensi hizi bila maneno yaliyopigiwa mstari:-** (i) Mwanafunzi ambaye alituzwa ni wa shule yetu

(ii) Sikuziona nyuzi ambazo huzitengeneza ngoma ambayo huiona pale

(g) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vielelezo vya vishale:**

Kiarie ni mwanafunzi mtiifu

(h) **Bainisha ngeli za nomino hizi :-**

(i) Kisu

(ii) Nyavu

(iii) Chai

(i) **Ainisha viambishi katika neno lifuatalo :-**

Kilichokikata

(j) **Nyambua kitenzi 'oa' katika hali tatu zifuatazo: tendewa, tendwa, tendea**

(k) **Eleza matumizi manne ya nukta**

(l) **Onyesha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo:**

Kamau alimlimia mamake shamba kwa trekta

(m) **Unda nomino kutokana na vitenzi hivi:-**

(i) Chapa (ii) Goma

(n) **Tambua kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii :-**

Chakula ambacho ni muhimu, huweza kujenga au kobomoa mwili wako.

(o) **Sahihisha sentensi ifuatayo:**

Ukienda mle pao atakuweko

(p) **Andika sentensi ifuatayo katika udogo:**

Mbwa mdogo amekanyagwa na gari.

## MTIHANI WA 39

(a) **Andika katika usemi halisi**

Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo

(b) **Andika kwa umoja**

Uovu waliotuonyesha hautasahaulika

(c) Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo: (i) Pamba

(ii) Bamba

(d) Sauti zifuatazo hutamkiwa wapi?

(i) /f/ (ii) /v/

(e) Onyesha matumizi **manne** ya kistari kifupi

(f) **Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo**

(i) Nafsi ya tatu umoja

(ii) Wakati uliopita (iii) 'O' rejeshi

(iv) kitendwa

(v) mzizi

(vi) kiishio

(g) **Tambulisha aina za vitenzi vilivyotumika katika asentensi hizi**

(i) Kazi hii ni nzuri.

(ii) Mazingira **yamekuwa yakihifadhiwa.**

(h) Pigia mistari chini ya viwakilishi katika sentensi zifuatazo

(i) Ambaye ni mjinga hatafaa kwa shughuli hizi (ii) Nani anaye huzunisha?

(i) Ngeli ya LI-YA hujumulisha nomino za vitu vya aina mbalimbali. Toa mifano **minne** ambayo ni tofauti na uelezee

(j) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo na ueleze ni shamirisho ya aina gani? Wazazi wanalipia watoto karo kwa hundi;

(k) Neno **'tikiti'** hupatikana katika **ngeli mbili** tofauti. Taja ngeli hizo na utunge sentensi (l) **Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale.**

Hakimu alimwadhibu kinyama.

(m) Nyambua vitenzi hivi kulingna na kauli ya kutendua na kutenda

| Kutenda | Kutendua | Kutendama |
|---|---|---|
| Ficha | | |
| Tanda | | |

(n) Ni nini maana ya neno kirai ?

MTIHANI WA 40

(a) Kati ya nomino za Kiswahili taja **ngeli mbili** ambazo nomino zake hazibadiliki katika umoja na katika wingi. Kisha utoe mfano mmoja kwa kila ngeli

(b) **Yakinisha:** Waumini wale hawaimbi wala hawaombi

c) **Andika kwa umoja**

Nguo zile uzionazo zilinunuliwa Ulaya

(d) Taja na kutolea mifano aina nne za silabi za Kiswahili

(e) **Unda nomino moja kutokana na nomino hizi**

(i) Mtu. (ii) Mhasibu..



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

(f) **Andika kwa ukubwa**

Kipaka hiki hakitosheki kwa maziwa haya kimezoea kipanya

(g) Onyesha shamirisho kipozi na shamirisho kidondo katika sentensi hii:-

Mama amempikia moto chakula kizuri

(h) **Tunga sentensi ya neno moja inayoonyesha sehemu zifuatazo**:-

(i) Kiambishi kikanushi nafsi

(ii) Kiambishi kiwakilishi cha hali timilifu

(iii) Kiambishi kiwakilishi cha kitendwa (nafsi)

(iv) Kauli

(v) Kiishio

(i) **Sahihisha sentensi hii kwa njia tatu tofauti**

Mtoto mwenye alicheza ameteguka

(j) **Andika visawe vya maneno haya**

(i) Rabsha..... (ii) Damu..

(k) Jaza mchoro ufuatao kwa irabu inayofaa

(l) Tunga sentensi ukitumia **'ni'** kama

(i) kitenzi (ii) kielezi

(m) Andika katika msemo halisi

Johana alisema kuwa angepata alama zote katika majaribu ya wiki iliyotangulia

(n) Tumia **'O'** Rejeshi ya mazoea katika sentensi ifuatayo;

Jembe ambalo lilinunuliwa limepotea

(o) Changanua ukitumia mtindo wa mishale

Mtoto anayelia sana ameadhibiwa leo asubuhi

(p) Onyesha matumizi mawili katika sentensi ya alama (') (q) Wafuatao wana ulemavu upi?

(i) Toinyo . (ii) Huntha ..

## MTIHANI WA 41

(a) Andika vinyume vya vitensi vilivyopigwa mistari

(i) Alikashifiwa kwa kazi aliyofanya

(ii) Kuimba kulifurahisha hadhira

(b) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi

(i) Abiria waliojeruhiwa sana walipelekwa hospitali haraka

(c)Eleza maana **mbilimbili** za sentensi zifuatazo ;

(i) Bibi yake amefika

(ii) Alimpigia mpira

(d) Kwa kutoa mifano, onyesha namna mbili vile kiambishi –j- hutumiwa (e) irabu **a, i,** na **u** hutamkwa wapi kwenye ulimi?

(f) Kamilisha na kueleza maana ya methali hii

(i) Mfinyanzi -.....................................

**(g) Andika usemi huu kwa usemi wa taarifa**

"Kefule! Mtoto huyu ni kaidi kama kirongwe. Hamheshimu babake!" alisema mzee Kamau.

**(h)** Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentenzi ifuatayo

**(i)** Darasa lililojengwa limefunguliwa rasmi

(ii) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo;

**(j)** Kanusha sentensi ifuatayo kwa udogo

(i)Mbuzi wake ana manyoya mengi na harufu kali

**(k)** Onyesha maana **mbili** ya neno taka (ala. 2)

**(l) Andika kwa umoja** (ala. 2)

(i) Tumewaondoleeni matatizo yenu, yafaa mtushukuru

(m) Eleza maana ya misemo:- (ala. 2)

(i) Fuga mtu – (ii)

Kuwa na faragha -

(n) Panga nomino hizi katika ngeli mwafaka (ala 2)

(i) Kipofu- .

(ii) Uyoga- .

(o) Bainisha viwakilishi katika sentenzi kisha useme ni vya aina gain. (alama

i) Mimi nitaondoka kesho

(ii) Huyo alichaguliwa na wengi

## MTIHANI WA 42

(a) Tumia kiulizi kifaacho kukamilisha maswali yafuatayo:

(i) Waashi wale wanaishi kwa

(ii) Mtoto alitaka majina…

(iii) Wanitania hivyo

(b) Tambua mzizi katika neno:

Tuliwalimia :

(c) Andika sentensi **tatu** ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii

Pale ndiko alimoingia

(d) (i) Nini maana ya yambwa (shamirisho)

(ii) Taja aina ya yambua iliyoipigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:

**Mama amempikia baba wali kwa sufuria**



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

(e) Neno "**mlango**" lina maana ya "uwazi wa kuingilia nyumba." Tunga sentensi **mbili** kubainisha matumizi mawili ya neno hili

(f) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya **"ndivyo"**

(g) Chai hiyo iliwavutia watahi (*Anza* : **Watahi…………..**) (al. 2)

(h) Tumia neno **"haraka"** katika sentensi kama: (al. 2)

(i) Nomino (ii) Kielezi

(i) Andika maana **mbili** za sentensi:

(i) Nenda ukamwone mwenyewe, usiogope.

(j) Onyesha maana za '**ni**' zilizopigiwa mstari

Nihamrishe "**Tokeni darasani**"

(k) Atakapokuja atamletea mlinzi uta na upote

(l) Maneno hayo yako katika ngeli gani?

(i) Ridhaa (ii) Nanasi

(m)Andika mifano ya sauti zenye sifa zifuatazo:

(i) Kipasuo cha kaakaa laini (ii) Nazali ya ufizi

(n) Tumia neno **"ngali"** kutunga sentensi kuonyesha

(i) Kitenzi kisaidizi (ii) Kitenzi kishirikishi

(o) Tumia kirejeshi kuonyesha mazoea katika sentensi ifuatayo:

(i) Mtoto anayelia ni huyu (ii) Neno maana ya kiwakilishi?

(q) Tambulisha viwakilishi katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani?

1.Nani alikukasirisha?... 2. Huyu huwashinda wote

(r) Tunga sentensi **moja** itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano

## MTIHANI WA 43

(a) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi

(i) Kishirikishi kipungufu

(ii) Kikuu

(b) Akifisha

je, unaipenda hali ilivyo mwenzake alitaka kujua

(c) Eleza matumizi ya '**ka**' na '**hu**' katika sentensi zifuatazo.

(i) Nilienda kanisani nikamkuta, nikamwamkua, nikamwomba msamaha. (ii) Baba hufika nyumbani usiku wa manane

(d) Yakinisha sentensi ifuatayo :

Mama hakutuchapa, hakutupa chakula wala maji

(e) Tofautisha kati ya sauti ghuna na sauti si ghuna huku ukitolea mifano miwili kwa kila aina

(f) Tunga sentensi mbili kutofautisha matumizi ya vitate hivi: Dua na tua

(g) **Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo wingi**



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

Njia nyembamba ni hatari kwa usafiri wa gari

(h) **Changanua sentensi ifuatayo ukitumia matawi**

Mzee ambaye hukuza pamba amefaidika sana

(i) **Ainisha mofimu zinazojitokeza katika kitenzi hiki**

Waliochekeshwa

(j) **Andika sentensi zifuatazo kulingana na kauli ulizopewa katika mabano**

(i) Ugonjwa wa saratani hufanya watu **wafe** polepole. (kauli ya kutendesha)

(ii) Mkulima **alisuka** kamba ndefu. (Kauli ya kutendata)

(k) **Tunga sentensi moja inayojumulisha sehemu hizi, Ala, kipozi, kitondo na chagizo**

(l) Neno kijana linaweza kutumiwa kama kivumishi au nomino, tunga sentensi kudhihirisha***U**

(i) Kivumishi

(ii) Nomino

(m) **Sahihisha sentensi zifuatazo**

(i) Mtoto ambaye aliyekuwa anacheza ameanguka.

(ii) Vitabu hizi ambazo zimesahihishwa ni za wanafunzi.

(n) Tunga sentensi mbili ukitumia vielezi vya namna mfanano na viigizi.

(o) Bainisha maneno yafuatayo yapo katika ngeli gani kisha tunga sentensi mwafaka:

(i) Manukato (ii) Uwati

(p) Eleza maana ya methali ifuatayo:

"Avunjaye nazi ni lazima aafaidi tui.

## MTIHANI WA 44

A) **Eleza maana mbili za:**

Mwanaida alikwenda sokoni peke yake.

B) **Akifisha sentensi hizi.**

i) Hodi hapana wenyewe nini Juma alimwaka nitarudi kesho.

C) **Andika maana ya methali ifuatayo.**

Achanikaye kwenye mpini hafi na njaa.

D) **Tumia "O" rejeshi katika sentensi hii.**

Mwanafunzi ambaye hudurusu ndiye hupita mtihani.

E) **Andika sentensi ifuatayo kwa kunyambua maneno yaliyo kwenye mabano kwa usahihi.**

Dhambi za mwanadamu zilim___________ (fa) Bwana Yesu. F)

**Eleza maana ya misemo ifuatayo.**

i) Teka bakunja.

G) **Taja maana ya maneno yaliyopigwa mistari.**

Tulipogawa mkate kila mtu alipata sehemu moja kwa nane tu kwani tulikuwa wanane H)**Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maelezo.**



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892

i) Sikusoma kwa bidii ndiposa sikufaulu katika mtihani ule.

(Anza: Ningalisoma ……………………………………….)

ii) Anakuja (andika katika wakati ujao hali timilifu) I)

**Eleza maana ya neno chungu kama lilivyotumiwa katika sentensi zifuatazo.**

i) Chungu yule ni mkubwa.

ii) Chungu kile ni kikubwa.

J) **Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo kama vivumishi.**

i) Sote. i) Zote.

K) **Andika nomino mbili kutokana na kitenzi safari.**

L) **Tumia viunganishi mwafaka kuunganisha sentensi hizi ziwe sentensi moja.**

Alikimbia kwa nguvu zake zote. Alishindwa, kulikuwa na mtu mwenye mbio kumliko.

M)**Eleza maana ya matumizi ya "ka" katika sentensi ifuatayo.**

Aliingia ndani, akaoga, akala kisha akalala.

N)**Taja sauti mbili za ving'ong'o**

O)**Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.**

Juma ameinjika chungu mekoni.

P) **Andika sentensi ifuatayo katika wingi wa udogo.**

Mtu/ mchoyo hamfai mwingine kwa vyovyote vile.

Q) **Kanusha sentensi hii;-**

Ukionana naye mwambie aje anione.

R) **Eleza na udhibitishe kwa mfano, matumizi mawili ya tu.** S)

**Changanua sentensi ifuaatayo kwa kielelezo visandu.**

Mwanafunzi aliyeleta kitabu chake amepongezwa

T) **Bainisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo**

Soroveya atapima wanunuzi viwanja. U)

**Nomino zifuatazo ni za ngeli gani?**

i) Insi … ii) Soksi

MAKALA HAYA



Kwa majibu, wasiliana na Bi.Mariam-0746711892